Alhamisi Novemba 19, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580404

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710


ama

ALHAMISI NOVEMBA 19, 2020 AFYA NA MAZINGIRA

Ukurasa 12
Umma wafunguka macho ukatili jinsia unavyowamaliza afya zao

Ukurasa 14
Wazalishaji Coca-Cola rasmi kusafisha fukwe unaochafuliwa na utitiri plastiki

## Majeruhi wa ajali gari kupinduka mara 3 alivyopewa maisha mapya

• Hajiwezi...'yaleyale' arejeshewa ukapera
• Mwanasheria trafiki aanika hali kitaifa

Na Beatrice Shayo

ALHAMISI wiki iliyopita, safu hii ilikuwa na mkasa wa majeruhi wa ajali kuanguka ghorofani. Leo ni simulizi ya mkasa unaofanana, safari hii ajali ya barabarani. Fuatilia:

"Nilivyopata ajali huduma ya kwanza ilikuwa ni kikwazo cha mimi kupata madhara makubwa katika mwili wangu, anayeniokoa hana uelewa wa kumsaidia mtu aliyepata ajali wananivuta kumbe wanazidi kuniongezea tatizo".

Ni maneno ya Abdulaziz Shamba. Ilikuwa mwaka 2003 alipokuwa safarini kulekea mkoani Tanga, gari lake lilipinduka mara tatu na akapata madhara shingoni na kuvunjika.

"Huduma ya kwanza pale tulipopata ajali ilikuwa shida, watu walikuwa wanafikiria kuiba na sio kutusaidia. Aliyekuwa anahangaika ni dereva wangu, mimi nilikuwa nimefunga mkanda gari ilivyopinduka ukawa unanibana kwenye shingo.

"Kutokuelewa kwa dereva, alikuja kunivuta akachangia hali yangu kuwa mbaya kiasi hiki, hakuwa na elimu ya kumsaidia aliyepata ajali," anasema Shamba.

Shamba, ambaye ni Katibu Mkuu wa Chama cha Watu Walioumia Uti wa Mgongo, anasimulia eneo alilopata ajali lilikuwa kijijini na hapakuwapo huduma za afya jirani.

Anasema licha ya gari kuwa na vifaa vipya, zikiwamo matairi, anahisi chanzo kikuu cha ajali kilikuwa mwendo kasi. Hata hivyo, hakufafanua.

"Basi...lilinipakia na kunipeleka kituo cha afya, nilivyofika pale mwanajeshi mmoja akiwa eneo hilo aliniona, akasema kwa hali yake apatiwe rufaa apelekwe Hospitali ya Muhimbili.

"Pale kijijini hapakuwapo gari la kubebea wagonjwa, bahati nzuri fahamu zilivyonijia, niliulizwa namba ya simu nikataja namba ya mtu wa ofisini Tanga," anaeleza Shamba, wakati huo akiwa meneja katika kampuni ya mafuta.

Anaeleza, mfanyakazi mwenzake aliyekuwapo Tanga aliwasiliana na Hospitali ya Rufani Bombo, alikosa gari kwa sababu iliyokuwapo haikuwa na uwezo kusafiri hadi Dar es Salaam.

SAFARI MUHIMBILI

"Ilikuja kupatikana Hiace (basi dogo) ya mtu binafsi wakatoa viti wakaweka godoro, wakatupakia kutuleta. Nimepata ajali saa tisa alasiri Muhimbili tumefika saa sita usiku," anaeleza.

Shamba anasema Tasisis ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI) ilikuwa haijaanza matibabu ya shingo, hivyo alikaa wodini kwa siku 14 madaktari wakijadiliana namna ya kumsaidia.

Anasimulia kipindi hicho alipatiwa dawa za kupunguza maumivu na baada ya siku 14, ukafikiwa uamuzi apelekwe nchini Afrika Kusini kwa matibabu zaidi na alipofika huko, alijulishwa amecheleweshwa matibabu kwenye huduma za awali.

"Nimeambiwa huduma ya kwanza nilitakiwa kutenganishwa sehemu niliyoumia ambayo sikupatiwa hadi nilivyofika Afrika Kusini. Hapa nilivalishwa ya shingoni (neel cap) hawajatenganisha ile mishipa ndio maana nimepata madhara zaidi," anasema.

Shamba, wakati huo alikuwa Katibu Mkuu wa Klabu ya Moro United na ndoto yake ilikuwa kufanya kazi u kocha wa soka, fani aliyosomea nchini Sweden na hadi anapata ajali, alikuwa na siku 12 tangu kurejea nchini, ndoto hizo zikatoweka.

Anasmulia kiafya, walimshauri na kumsaidia kurudia maisha ya kawaida, ingawa hajaweza kutekeleza vilivyo, kutokana na ulemavu wa sasa.

Anadokeza shida inayomkabili sasa, akieleza:"Ofisi ilikuwa inakutibia, wanakutegemea upone urudi ofisini. Wanaona muda unazidi kwenda hauponi na wao walifika wakati wakachoka na kukata tamaa kunitibia."

BAADA HOSPITALI

Kifamilia, anajitambulisha alikuwa na mke na watoto wawili, ambao sasa ni wanachuo cha elimu ya juu nchii na mkewe, waliopata ajali wote, Shamba analalamika kukimbiwa na mwenza huyo, katika maisha baada ya ajali.

"Mimi nina familia, inanibidi niwahudumie watoto wangu licha nipo katika hali hii. Gari inavyopata ajali nilikata bima ndogo hawakuweza kunilipa,"anasema.

Mtaalamu wa Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), Dk. Lutfi Abdallah, anasema mtu anavyopata ajali mbaya, muokoaji asipomnyanyua vizuri, kuna uwezekano wa madhara zaidi, hata kifo.

"Kuna nchi nyingine mtu amepata ajali wanavyokuja askari ama zimamoto au waokoaji, wanaelewa jinsi ya kukubeba, ili asimsababishie madhara mgojwa aliyepata

Abdulaziz Shamba, majeruhi wa ajali ya barabarani, akisimulia kilichomsibu. PICHA: BEATRICE SHAYO.

Endelea Uk. 12

UKURASA 11

**CHADEMA**, ACT-Wazalendo zajitoa uchaguzi madiwani

UKURASA 2



**OFISA** wa LATRA afunguliwa kesi ya ya kutumia silaha

UKURASA 9

# Mtoto aliyelelewa na nyani atamka maneno

UKURASA 2



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akiangalia sehemu ya ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), mkoani Pwani jana na alishuhudia tukio la uchepushaji wa maji ya Mto Rufiji kwenye handaki, ili kupisha ujenzi wa tuta kuu la bwawa la kufua umeme. **PICHA: OWM**

# Safari treni mwendokasi sasa kuanza rasmi Aprili

UKURASA 2


## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**MWINYI ATETA NA WAFANYABIASHARA KUHUSU KUHAMISHWA**
SIKU tatu tu baada ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Hassan Khatib, kuwataka...

UKURASA WA 4

**MATUMIZI HOLELA 'ANTIBIOTIC' YASABABISHA USUGU MWILINI**
MATUMIZI holela ya dawa za antibiotic (kiuavijasumu) yameelezwa kusababisha usugu...

UKURASA WA 4

**ATM KUBADILISHA FEDHA ZA KIGENI YAZINDULIWA**
BENKI ya NMB imezindua mashine ya kutolea fedha (ATM) ya kwanza nchini yenye uwezo wa kubadili fedha za kigeni ambayo itakuwa...


## RC ataka mkutano mwafaka wa saruji

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA SC WAANZA KUSHIKANA 'UCHAWI' UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6

# CHADEMA, ACT-Wazalendo zajitoa uchaguzi wa udiwani

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na ACT-Wazalendo, vimejitoa katika uchaguzi wa udiwani kata ya Igumbilo, Manispaa ya Iringa uliopangwa kufanyika Desemba 8, mwaka huu.

Kata hiyo haikufanya uchaguzi katika uchaguzi mkuu uliofanyika nchini Oktoba 28, baada ya kifo cha mgombea wa CCM kutokea Oktoba 16, hivyo kusababisha Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuuahirisha.

Kutokana na kujitoa huko, Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo la Iringa Mjini, Hamid Njovu, jana alimtangaza Boniface Kilave kuwa mshindi wa udiwani wa kata hiyo baada ya kupita bila kupingwa.

Novemba 13, NEC kupitia Kaimu Mkurugenzi wa Uchaguzi, Gerald Mwanilwa, alitangaza kufanyika kwa uchaguzi mdogo kwenye kata tatu ikiwamo hiyo.

Kata zingine ni Nyahanga iliyoko Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga na Kibosho Kati, kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, mkoa ni Kilimanjaro.

Katika kata hiyo ya Igumbilo, wagombea ambao ni Wilbert Kilave (CHADEMA) na Mahamad Rassa (ACT- Wazalendo), walitangaza kujiondoa katika kinyang'anyiro hicho.

Njovu alisema wagombea hao waliwasilisha barua zao za kujitoa kugombea zikiambatanishwa na viapo vyao vya tamko la kujitoa vilivyotolewa mbele ya hakimu juzi.

Alisema barua hizo za kujiondoa zilizingatia kifungu cha 50 cha sheria ya uchaguzi wa serikali za mitaa, sura ya 292 ya mwaka 2015 na kanuni zake.

Alisema diwani mteule atapatiwa hati ya kuchaguliwa kwenye nafasi hiyo ifikapo Desemba 8, ambayo ni siku iliyopangwa kufanyika uchaguzi huo.

Kwa mantiki hiyo, CCM imeshinda kata zote 18 za Jimbo la Iringa Mjini na kufanya Baraza la Madiwani pamoja na Halmashauri ya Manispaa ya Iringa kuongozwa na chama tawala.

Katibu Kata ya Mkwawa, Halid Abdalla, alisema baada ya udiwani huyo kuthibitishwa, wataelekeza nguvu kata zote ili kuhakikisha wananchi wanapata maendeleo.

Katika taarifa ya NEC ya Novemba 13, NEC kupitia Kaimu Mkurugenzi wa Uchaguzi, Mwanilwa alitangaza kuwa kampeni za uchaguzi huo mdogo zitafanyika kwa siku 21 kuanzia juzi hadi Desemba 7 na siku itakuwa ni ya uchaguzi.

Taarifa hiyo ilisema kuwa NEC imepanga kufanya uchaguzi Kata ya Kibosho baada ya wakati wa uchaguzi mkuu kukosekana karatasi za kura.

# Mtoto aliyelelewa na nyani aanza kuzungumza

**Na Richard Makore,** MWANZA

MABULA Bukombe, mkazi wa Jiji la Mwanza aliyelelewa na nyani porini tangu akiwa mdogo ameanza kuzungumza maneno machache baada ya kuchangamana na watoto wenzake kwa zaidi ya miaka minne.

Akizungumza na Nipashe katika kituo cha kulelea watoto yatima cha Upendo Daima cha jijini Mwanza, Ofisa Ustawi wa Jamii, Paul Ligali, alisema mtoto huyo kwa sasa ameanza kutamka maneno machache yakiwamo ya utani.

Alisema mtoto huyo aliokotwa na nyani katika Wilaya ya Bukombe, mkoani Geita na kupelekwa porini akiwa mdogo na kuanza kuishi naye kama mwanawe.

Akiwa porini alijifunza tabia na kuongea kama nyani ikiwamo kula matunda pekee.

Ligali alisema, mtoto huyo alilelewa kwenye mikono ya nyani, baada ya mchungaji wa ng'ombe kumwona na kwenda kutoa taarifa kijijini kwao.

Baada ya taarifa hiyo, alisema askari wa wanyamapori walikwenda kumsaka na kufanikiwa kumwokoa mtoto huyo na kumpeleka ustawi wa jamii.

Alisema wakati mtoto huyo akiokolewa kutoka mikono ya nyani alikuwa hawezi kuzungumza na alikuwa akilia kama mnyama huyo.

Kadhalika, alisema tabia aliyokuwa nayo miaka minne iliyopita ilikuwa ni pamoja na kukataa kula chakula na badala yake kuomba matunda kwa kutumia ishara ya mikono.

Ofisa huyo alisema alipompokea mtoto huyo aliyekadiriwa kuwa na miaka sita, alikuwa hawezi kuzungumza chochote.

Alisema, baada ya kuishi na watoto wenzake kwa takribani miaka minne sasa ameweza kutamka neno moja moja na kucheza nao.

Alisema mtoto huyo ameshindwa kuanza shule kwa kuwa hawezi kuzungumza vizuri licha ya kukadiriwa kuwa na umri miaka 10 hivi sasa.

Aliomba jamii kufika katika kituo hicho cha Upendo Daima (Back Home House) ili kumtambua kwa kuwa mpaka sasa hawajapata wazazi wake.



Makamu Mwenyekiti wa CCM, Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akiongoza kikao cha kamati maalum ya Halmashauri Kuu ya chama hicho, katika Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui jana. Katikati ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**.

# Reli ya kisasa kuanza rasmi Aprili

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema ameridhishwa na kasi ya ujenzi wa kipande cha reli ya kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro ambacho kimekamilika kwa zaidi ya asilimia 90 na kuwaahidi Watanzania kuwa njia hiyo itapitisha treni ya abiria kwa mara ya kwanza Aprili, mwakani.

Alisema hayo wakati alipotembelea ujenzi wa stesheni ya reli ya treni ya mwendo kasi, Morogoro eneo la Kihonda na kwamba ndoto na matamanio ya Rais John Magufuli ni kuona miradi mikubwa ya kimkakati ukiwamo wa SGR na wa umeme wa Julius Nyerere unakamilika.

"Waliokuwa hawaamini sasa wataamini, nimeshatembelea kituo cha Tanzanite Stesheni Dar es Salaam, abiria wa treni watapanda ghorofani ili kupanda treni, karakana ya Soga, na nikapanda treni kutoka Soga hadi Pugu, sasa zimebaki kama kilometa hamsini hadi sitini kukamilika, ili mtu aweze kutembea kwa treni kutoka Dar hadi Morogoro, na zaidi kiberenge kitaanza kutumia reli hii ifikapo Desemba, mwaka huu," alisema.

Majaliwa alisema kilichobaki kwa sasa katika stesheni ya Morogoro ni kuweka njia za umeme, ili reli hiyo ianze kazi Aprili mwakani badala ya Desemba, mwaka huu kama ilivyopangwa awali.

Alisema kuchelewa kidogo kukamilika kwa mradi huo kulisababishwa na janga la corona hasa kwa nchi zingine duniani.

"Ujenzi huu unategemea vifaa na malighafi zingine kutoka nje ya Tanzania, kwa hiyo corona ilisababisha usafirishaji wa mizigo kutoka nje kuathirika, ujio wa wataalamu zaidi kuongeza nguvu kutokana na mipaka kufungwa, ingawa hali hiyo haikuathiri mwenendo mzima wa mradi kama ulivyokusudiwa," alisema Waziri Mkuu.

Pia, alisema kukamilika kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro kutafungua na kuboresha fursa kubwa za shughuli za kiuchumi na badala ya msafiri kutumia saa tatu kutoka Morogoro hadi Dar es Salaam, atatumia saa moja na nusu.

Alisema stesheni hiyo itakuwa na uwezo wa kuingiza na kutoa watu takribani 800 kwa siku, magari zaidi ya 150, bodaboda na shughuli zinginezo, hali itakayowafanya watoa huduma katika nyanja mbalimbali kufanya biashara na shughuli nyingine za kujikwamua na umaskini.

Aliwahimiza wafanyakazi wa mradi huo kutoka kampuni ya Yepi Merkezi, kujifunza kitaalamu maelekezo ya kila hatua, ili kampuni hiyo ya kigeni ikiondoka, waweze kushiriki kufanya matengenezo yanapohitajika badala ya kutegemea wataalamu wa kigeni kuja kusaidia matengenezo madogo.

Wakati huo huo, ameliagiza Jeshi la Magereza Tanzania na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kupeleka ofisini kwake, vielelezo na nyaraka zote halali za kuonyesha umiliki wa maeneo yanayogombaniwa jirani na stesheni hiyo ifikapo Novemba 28, mwaka huu na kipindi cha mpito, mtu au taasisi yoyote isijihusishe na ujenzi hadi serikali itakapotoa maamuzi.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli nchini (TRC), Masanja Kadogosa, alisema kukamilika kwa stesheni hiyo kutawezesha watu 800 kupata huduma kwa wakati mmoja kwa kuingia na kutoka na kwamba hadi sasa kuna uwezekano wa kutembea kilometa 145 kwa treni kutoka Dar es Salaam na kilometa 60 zimebaki kwa maana ya utandikaji reli kutoka kituo cha Pugu kufika Morogoro.

Alisema miundombinu ya umeme imefanikisha kwa asilimia 74, ujenzi wa madaraja likiwamo la Dar es Salaam lenye urefu wa kilometa tatu ambalo limekamilika kwa asilimia 91.75.

Kadogosa alisema kazi kubwa iliyobaki ni ujenzi wa fensi kuzunguka njia ya reli, inayotarajiwa kutumia kati ya miezi mitatu hadi minne hadi kukamilika na utandikaji wa reli kwa kilometa 145 umeshafanyika wakiwa katika hatua za mwisho.

## HABARI KITAIFA

# Mwinyi ateta na wafanyabiashara kuhusu kuhamishwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SIKU tatu tu baada ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Hassan Khatib, kuwataka wafanyabiashara wa eneo la Kijangwani kuondoka, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, jana alikutana na kuteta nao.

Akizungumza na wafanyabiashara hao katika eneo hilo, Rais alisema kitendo cha kuhama kutoka eneo moja kwenda lingine kunasababisha kufa kwa mitaji yao ya biashara lakini hatua hiyo haina nia mbaya dhidi yao.

Rais Mwinyi aliutaka uongozi wa serikali ya mkoa, Baraza la Manispaa na wafanyabiashara kukaa na kutafuta sehemu ya kudumu itakayokuwa nzuri ili kuwawezesha kufanya biashara zao kwa urahisi.

Alisema kukaa pamoja kutasaidia kutafuta sehemu nzuri ikiwamo miundombinu bora ili kuwawezesha wafanyabiashara hao kufanyabiashara vizuri.

Dk. Mwinyi alisema wote wanafahamu soko hilo si la kudumu na lipo kwa muda na kuwataka kipindi hiki cha kutafuta eneo lingine kubaki hapo hadi sehemu itakapopatikana.

Alisema Ilani ya Chama cha Mapinduzi imesema itaweka mazingira bora ya wafanyabiashara na kuwapa vitambulisho ili kodi zisitolewe kila siku, hivyo akasisitiza kuwa ahadi aliyoitoa ipo kwa kuona mazingira yanakuwa mazuri ya kufanya biashara.

"Nakuahidini nitakuwa wa kwanza kulisimamia suala hili kwani nimeahidi na nimekuja hapa nitakuwa wa kwanza kulisimamia hili," alisema huku akishangiliwa na wafanyabiashara hao.

Akizungumzia ujenzi wa kituo cha magari ya abiria Kijangwani, alisema mradi huo una lengo la kuwawekea mazingira mazuri ya biashara, hivyo wafanyabiashara hao hawana budi kukubali ili kuwapo kwa mazingira mazuri.

"Nauagiza uongozi wa Mkoa wa Mjini Magharibi kuharakisha kutafuta eneo ambalo litakuwa la kudumu wa wafanyabiashara. Kama hamuwezi kulipata mimi nitalipata," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Juma haji alisema: "Hatukatai kuhama katika soko hili ila tunaomba tutafutiwe sehemu iliyo nzuri maana kuhamahama huku kunatuathiri sana.

Alisema kipindi cha corona waliondolewa katika soko la Darajani na kupelekwa eneo la Kijangwani ambako wengi walipoteza mitaji na kushindwa kuendelea na biashara.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack akikagua bei ya saruji kwenye maduka na maghala mbalimbali mkoani humo jana. **PICHA: MARCO MADUHU.**

# RC ataka mkutano mwafaka saruji

**Na Waandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameshauri Wizara ya Viwanda na Biashara, kuwakutanisha wakuu wa mikoa, wadau wa usambazaji na wenye viwanda ili kujua mzizi wa tatizo la saruji .

Katika mahojiano na mwandishi wa gazeti hili, Chalamila, alisema bidhaa hiyo imeadimika katika maeneo mengi na wafanyabiashara wanasema wakiagiza hawaipati na wakati mwingine inachukua muda mrefu kupata.

Alisema ni lazima ufanyike mkakati wa kuona namna gani ya saruji na vifaa vingine vya ujenzi vinawekeza utaratibu mzuri wa uzalishaji na usambazaji kama vilivyo vinywaji baridi na moto ambavyo havijaadimika mtaani wala kupanda bei bila utaratibu.

"Nashauri wizara iwaite wakuu wa mikoa na wadau wa usambazaji na wenye viwanda ila kusema katika kikao ili kujua tatizo," alisisitiza.

Mkuu huyo wa mkoa alisema katika utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alichobaini ni wauzaji kukosa bidhaa hiyo kutoka viwandani.

Chalamila alisema katika ufuatiliaji alioufanya katika mkoa wake, amebaini mambo kadhaa yaliyosababisha kuwapo kwa kero kubwa kwa wananchi juu ya saruji kuwa ni pamoja na uzalishaji wa viwanda kutoendana na mahitaji ya soko.

"Hapo ndipo tatizo tatizo lilipoanzia. Tatizo dogo la pili ni wafanyabiashara kutumia fursa ya uhaba wa saruji sokoni kupandisha bei," alisema.

Chalamila alisema kiwanda cha saruji Mbeya, kwa mfano, kwa mwaka kimekuwa na uwezo wa kuzalisha saruji tani milioni moja kwa mwaka.

**KATAVI**

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera, alisema kuwa kamati za usalama za wilaya na mkoa zimefuatilia na kubaini tatizo kubwa ni wenye viwanda kupunguza uzalishaji, hivyo wasambazaji wengi kukosa mzigo wa kutosha.

Alisema katika mkoa wake wamekusudia kuwaunganisha wafanyabiashara wakubwa wa saruji na viwanda ili kufuata saruji kwa bei ya viwandani na kuiuza kwa gharama nafuu.

Katika wilaya ya Mufundi, Mkuu wa Wilaya, Jamhuri Wiliam, alisema amezunguka kwenye maduka yote makubwa na kuchunguza kiwango cha saruji walichonancho na kuwapa onyo wafanyabiashara hao.

Alisema wako mawakala wakubwa sita ambao wanasambaza saruji na mawakala watano wana akiba ya saruji ila wakala mmoja hana kabisa.

Alisema bei zao ni kati ya Sh. 16,000 na Sh. 18,000 ikiwa ni ongezeko la Sh. 3,000 kutoka bei ya awali.

**SHINYANGA**

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, amesema ambaini sababu za wafanyabiashara kupandisha bei ya saruji na kupiga marufuku kuuza bei ya juu.

Mfuko wa Saruji mkoani humo unauzwa kati ya Sh. 20,000 na 22,000 kwa wafanyabiashara wa maduka, wakati bei halisi ni Sh. 17,500 hadi 18,000.

Akiwa katika Manispaa ya Shinyanga alibaini kuwa bidhaa hiyo ipo ya kutosha ila kuna ujanja ujanja kwa wafanyabiashara kutaka faida kubwa.

Mmoja wa wafanyabiashara, John Ngalya, alikiri kupandisha bei ya saruji kwa madai kuwa na wao wanauziwa bei ya juu kutoka kwa wanunuzi wakubwa wanaotoa viwandani.

Wakala wa kusambaza saruji kwa wafanyabiashara kutoka viwandani, Shufaa Mabula, alisema bei ya saruji imepanda kutokana na uzalishaji kuwa mdogo kwa oda jambo lilosababisha kuwapo gharama ya kusubiri mzigo.

**Imeandikwa na Francis Godwin (IRINGA) Na na Marco Maduhu (SHINYANGA)**

# Wapinzani washauriwa kutosusia Bunge

**Na Romana Mallya**

WACHAMBUZI wa siasa wamevitaka vyama vya upinzani kutosusia Bunge kwa madai ya uchaguzi haukuwa huru na haki badala yake wawatume wawakilishi bungeni ili wananchi wasikose sauti ya upinzani.

Wakitoa maoni yao jana kwa nyakati tofauti, wachambuzi hao walisema wanaamini hawajasusia bali wanatafakari namna ya kuwatuma wawakilishi hao bungeni.

Mchambuzi wa siasa, Deus Kibamba, alisema kuwa wanatakiwa kukosa mikutano mfululizo ili waweze kufukuzwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai.

"Kwa sasa wamekosa mkutano mmoja na wanatakiwa kukosa mitatu mfululizo bila kumtaarifu chochote Spika, wakifanya hivyo watafukuzwa bungeni, hizi ni kanuni za Bunge zinasema hivyo, hatujui kama watakosa mkutano wa pili na wa tatu," alisema.

Kibamba alisema wasipopeleka wabunge viti maalum moja ya athari zitakazotokea ni kwamba watalinyima Bunge sauti ndogo ambayo ingeweza kujitokeza bungeni.

"Kususia wameshashindwa kwa sababu mbunge wa CHADEMA aliyechaguliwa Nkasi, alishajiandikisha bungeni na wa CUF (Chama cha Wananchi) walihudhuria, unaweza ukasimama na kuiambia dunia kuwa mmesusia," alihoji.

Kibamba alisema kuwa, "Kwa sasa hawawezi kusimama mpaka wamfukuze kwanza mbunge au wabunge walioingia bungeni wa vyama vyao ndipo wataweza kuiambia dunia tumesusia na tumewafukuza."

Alisema upande wa hasara kwa upinzani utakuwa mkubwa zaidi kwa sababu nguvu yao ambayo tayari imemomonyolewa, itaendelea kuathirika zaidi kimapato.

"Mkiwa bungeni mnaweza kuendelea kuzuia sheria mbaya ambazo zinataka kupitishwa kwa kutoa hoja ya wizi hata kama hawatasikilizwa, lakini Watanzania watawasikia, kutokuwepo kabisa na kususia Bunge na Baraza la Wawakilishi na madiwani, kutaleta madhara zaidi kwa upinzani," alisema.

Aliwashauri badala ya kususia waanzishe vikao vya kutafakari anguko hilo la kwenye uchaguzi limetokana na nini, ili kama ni kura ziliibiwa ukusanywe ushahidi wa kwenda mahakamani au kuandika ripoti kuelezea zilivyoibiwa kura.

Alisema mpaka sasa upinzani unatoa maneno bila ya kuwa na ushahidi kamili kwamba katika jimbo gani ziliibiwa ngapi, zilibebwa kwenye gari namba ngapi, maboksi mangapi yalibebwa.

Mchambuzi wa siasa, Prof. Abdallah Safari, alisema endapo upinzani hautapeleka wabunge wa viti maalum maana yake, litakuwa ni bunge la CCM na sheria ya vyama vingi itakuwa haina maana.

Mwishoni mwa mwezi uliopita CHADEMA na ACT-Wazalendo vilitoa tamko la kutoutambua uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28 na kutaka urudiwe na kusimamiwa na tume huru.

NEC ilisema vyama viwili kati ya 20 vilivyoshiriki katika uchaguzi mkuu ambavyo ni CCM na CHADEMA, ndivyo vyenye sifa ya kupata wabunge wa viti maalum kwenye Bunge la 12.

NEC ilitoa idadi ya wabunge wa viti maalum ambapo CCM ilipata 94 na CHADEMA 19 na kwamba hadi sasa upinzani haujatoa majina yake.

# Matumizi holela ‘antibiotic’ yasababisha usugu mwilini

**Na Christina Mwakangale**

MATUMIZI holela ya dawa za antibiotic (kiuavijasumu) yameelezwa kusababisha usugu kwenye mwili wa binadamu.

Pia yameongezeka kufikia asilimia 50 hasa kipindi cha ugonjwa wa Covid-19.

Utafiti uliofanywa na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), ulibaini pia usugu wa dawa aina ya gentamicin ambayo inatibu magonjwa yanayosababishwa na bakteria, kama maambukizi ya njia ya mkojo (UTI), mafindo findo, umeongezeka kutoka asilimia saba mwaka 2003 na kufikia asilimia 44 mwaka 2011.

Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, alipokuwa akifungua wiki ya kukuza uhamasishaji na kuzuia usugu wa vimelea dhidi ya dawa duniani, inayoadhimishwa kuanzia Novemba 18 hadi 24, mwaka huu.

Alisema kuna ongezeko la matumizi holela ya dawa hizo bila kufuata ushauri wa kitabibu, huku baadhi wakizitumia kwa ajili ya kunenepesha mifugo kwa kuwachanganyia kwenye chakula hali inayosababisha vifo kwa binadamu.

“Ni hali ya kutisha zinatumika isivyo sahihi, dawa hizi zinajumuisha makundi ya kutibu fangasi, kufubaza virusi na protozoa maalum kwa ajili ya malaria, tangu wataalamu wa tiba walipogundua antibiotic, imesaidia kupunguza vifo kuwezesha wagonjwa kupona kwa asilimia 90 kutoka asilimia 10, hii inaonyesha mafanikio,” alisema Prof. Makubi.

“Matumizi ya dawa yasiyo sahihi kwa binadamu, wanyama madhara yake yanaweza kuwa ya kutisha, huathiri mazingira na mfumo wa vimelea dhidi ya dawa hizo. Dozi imalizwe isikatishwe,” alisema Prof. Makubi.

Alisema takwimu za Benki ya Dunia (WB), zinaonyesha watu 700,000 hufariki dunia kila mwaka kutokana na usugu wa dawa hizo.

“Utafiti uliofanywa Tanzania ulionyesha kuna usugu kwa wagonjwa wanaougua kifua kikuu (TB) kutokana na Erythromycin na amoxicillin, na malaria.

Prof. Makubi alisema kipindi walichokuwa na maambukizi ya virusi vya corona dawa aina ya Erythromycin na amoxicillin, mahitaji yalikuwa makubwa na kufanya dawa hizo kuadimika.

“Watu walitumia dawa za antibiotic bila kuandikiwa na madaktari hali ambayo ni hatari kwa afya zao.

Aliagiza viongozi, mamlaka za kusimamia dawa ikiwamo TMDA isimamie uingizwaji, usambazaji wa dawa nchini ili kupunguza matumizi hayo.

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) nchini, Dk. Tegest Mangestu, katika taarifa yake iliyosomwa kwa niaba yake na Rose Shija, alisema matumizi yasiyo sahihi ya dawa hizo kwa Afrika kipindi cha corona yalifikia asilimia 72.

Alisema utafiti ulibaini kati ya waliotumia dawa hizo ni asilimia nane tu walikuwa na uhitaji wa kitabibu wa dawa hizo.




Mkurugenzi wa Usimamizi wa Sekta ya Fedha kutoka Benki kuu ya Tanzania, Dk. Jerry Sabi, akifurahia fedha alizozitoa kwenye ATM mpya ya NMB yenye uwezo wa kubadilisha fedha za kigeni kuwa shilingi ya Tanzania, huku Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB Riuth Zaipuna, Ofisa Mwandamizi katika kitengo cha Ubunifu cha NMB, Gilbert Rurononа na Mkuu wa Kitengo cha Fedha za Kigeni, Jeremiah Lyimo wakishuhudia. NMB Jana ilizindua ATM maalumu yenye uwezo wa kubadilisha Dola ya marekani, Paundi ya Uingereza na Euro ya Umoja wa Ulaya kuwa shilingi ya Tanzania, ATM ambazo zitawekwa kwenye Viwanja vya ndege vya Dar es Salaam, Zanzibar na KIA. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# ATM kubadilisha fedha za kigeni yazinduliwa

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI ya NMB imezindua mashine ya kutolea fedha ya kwanza nchini yenye uwezo wa kubadili fedha za kigeni.

Imesema ATM hizo zitawekwa katika viwanja vya ndege vikubwa nchini ambavyo ni uwanja wa Kimataifa vya Julius Nyerere, Uwanja wa Kilimanjaro na ule wa Abeid Amani Karume, Zanzibar, ili ziweze kutumiwa na wasafiri wanaoingia na kutoka nchini wanaohitaji fedha za Tanzania au za nchi waendako.

“Mteja sasa anaweza kubadilisha fedha hadi kiasi cha Dola za Kimarekani 2,000 kwa wakati mmoja kwa viwango vya kubadilishia fedha vya Benki ya NMB,” alisema jana Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna.

Alisema wateja na wasio wateja wake wataweza kubadilisha fedha za kigeni kwa kutumia mashine mpya ya ATM zenye uwezo wa kubadili fedha.

“Tumeanza na Dola za Marekani, Euro za Umoja wa Ulaya na Pound ya Uingereza kubadilisha kwenda shilingi ya Tanzania,” alisema.

“Hii ina maana zoezi la kubadilisha fedha sasa litakuwa rahisi na haraka na hasa pindi mashine hizi zitakapowekwa kwenye viwanja hivi vya ndege, ambapo mteja anaweza kujihudumia mwenyewe kupitia ATM hizi za kubadili fedha za NMB.

“Tunaanza na aina hizo tatu za sarafu lakini muda sio mrefu tutaongeza na fedha za mataifa mengine,” alisema Zaipuna.

Alisema wamelifanyia kazi hili kwa weledi na ubunifu mkubwa na sasa tunakuja na suluhu ya teknolojia kuongeza nguvu ya upatikanaji wa huduma hiyo ambayo imekuwa ikitolewa na matawi yetu yote nchini, zaidi ya matawi 225

Mkurugenzi wa Usimamizi wa Sekta ya Fedha wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Jerry Wambura, aliushukuru uongozi wa benki ya NMB kwa kuwa mmojawapo wa anayeandika historia ya sekta ya benki hasa katika biashara ya kubadilisha fedha za kigeni.

“Nafurahi sana kuona leo NMB inazindua mashine ya kutolea fedha () ya kwanza nchini yenye uwezo wa kubadili fedha za kigeni za Euro, Paundi na Dola za Kimarekani kuwa shilingi za kitanzania,” alisema Wambura.

Alitoa rai kwa benki zingine nazo kufuata mfano huo na kuanza kutoa huduma kama hizo

## Viongozi wa dini waonya kuhusu uvunjifu amani

**Mwandishi Wetu,** KATAVI

BAADHI ya viongozi wa dini na chifu wa Kabila la Wabende Mkoani Katavi, wamekemea vikali vitendo vinavyofanywa na baadhi ya watu kwa lengo la kukwamisha mipango ya maendeleo inayofanywa na serikali kwa kupandikiza chuki miongoni mwa Watanzania, hususan vijana.

Onyo hilo lilitolewa jana sambamba na uzinduzi wa kampeni ya kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto uliofanyika mkoani hapa ukibebwa na kaulimbiu ‘Twende Pamoja, Ukatili Tanzania Sasa Basi’.

Viongozi hao walisema kutokomeza ukatili nchini kunaenda sambamba na kukemea kauli za baadhi ya watu wenye nia ovu wanaowachochea vijana kuichukia serikali yao kwa manufaa yao binafsi.

Kwa nyakati tofauti, walisema uchaguzi mkuu umekwisha na viongozi wamepatikana kwa haki na kama ilivyo katika vitabu vya dini, hakuna sababu ya kuendelea kuchochea chuki kwa lengo la kusababisha machafuko na badala yake kuheshimu mamlaka.

“Hivi karibuni tulikuwa na uchaguzi mkuu ambapo viongozi wetu wamepatikana kwa haki,wameapishwa na wanaendelea kutuongoza katika kuelekea uchumi wa juu.

“Asitokee mtu anayekusudia kuhujumu juhudi za serikali ambazo zimedhihirika kwa mambo mengi katika kipindi cha kwanza cha serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi wa Rais Dk. John Magufuli,” alisema Askofu Julius Mussa wa Makanisa ya Free Pentecost Church of Tanzania.

Alisema siku za karibuni kuna baadhi ya watu wanaotoa kauli zenye viashiria vya kuvunja amani ya nchi na hivyo kukwamisha maendeleo yaliyopatikana chini ya uongozi wa serikali ya awamu ya tano.

Pia alisema Rais Magufuli na timu yake tayari imejipambanua kwa kuongoza Watanzania kujiletea maendeleo na mambo mengi yaliyofanyika katika kipindi cha kwanza cha serikali ya awali ya tano yanaonekana bayana, hivyo hakuna sababu za kutumia propaganda chafu za kuhatarisha amani iliyopo. Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo, Katibu Mkuu,Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii), Dk. John Jingu, aliwataka Watanzania katika ngazi zote kuungana na kupinga vitendo vinavyolenga kuhujumu mipango ya serikali.

Katika hatua nyingine, Dk. Jingu alisimikwa kuwa mmoja wa machifu wa kabila la Wabende kwa kukabidhiwa zana za kimila ikiwa ni sehemu ya kutambua kazi anayoifanya hasa za kupambana na vitendo vya kikatili dhidi ya wanawake na watoto.

HABARI KITAIFA



Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Dk. Donald J. Wright, akikabidhi cheti cha ruzuku kwa Alphonsina Kanyeto, mmoja wa wanufaika wa Mfuko Maalum wa Balozi wa kusaidia miradi ya maendeleo inayoendeshwa na wanajamii wenyewe wakati wa hafla iliyofanyika nyumbani kwake, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: UBALOZI WA MAREKANI**

# Marekani yapiga jeki mil. 773/- miradi ya kijamii

**Na Edwin Mhagama**

UBALOZI wa Marekani kupitia mfuko wa kusaidia miradi ya maendeleo, umetoa ruzuku ya Sh. milioni 773.4 kwa miradi sita ya kijamii nchini.

Akitia saini makubaliano hayo jana nyumbani kwake jijini Dar es Salaam,††Balozi wa Marekani nchini, Donald Wright, alisema msingi wa mabadiliko katika jamii unatokana na wananchi wenyewe kuamua kujiunga kwa lengo la kuleta mabadiliko††kwenye jamii husika.

ìNinaamini mabadiliko ya kweli na ya kudumu hutokea pale ambapo wananchi katika ngazi ya chini kabisa hujiunga pamoja na kuleta mabadiliko chanya katika jamii zao,î alisema Balozi Wright.

Ruzuku hiyo imetolewa kwa vikundi, taasisi na asasi mbalimbali ambazo zimejikita katika masuala ya kijamii ikiwamo ujasiriamali, sheria, maendeleo ya jinsia na vijana, kilimo, elimu, walemavu, huduma ya maji safi na salama pamoja na uwazi na††utawala bora.

†Taasisi na asasi ambazo zimenufaika na ruzuku hiyo nchini zinapatikana katika mikoa mbalimbali††ikiwamo Njombe, Morogoro, Dodoma , Mara, Shinyanga na Mwanza.

Baadhi ya taasisi hizo na ile ya maendeleo ya kilimo na ufugaji (LAPDA), Taasisi ya Ujasiriamali ya KASEG na Shirika la Maendeleo ya Kilimo na††Ufugaji Musoma.

Zingine ni Taasisi ya maji safi kwa afya bora Ifakara (MSABI), Taasisi ya Mazao, Wajasiriamali na Ufugaji (PVL) na Thubutu (TAI), Kituo cha Msaada wa Kisheria kwa Wanawake, Taasisi ya Wajibu na kituo cha kisheria.

Tangu mwaka 1965, ubalozi wa Marekani nchini Tanzania kupitia mfuko maalumu wa balozi, umekuwa ukisaidia Watanzania katika miradi ya maendeleo inayoendeshwa na wanajamii wenyewe yenye lengo ya kujiongezea kipato pamoja na miradi endelevu.

# Wagonjwa wa akili wanatibika - Dokta

**Na Richard Makore**, MWANZA

DAKTARI bingwa wa magonjwa ya afya ya akili, Gema Sembeye, amesema wagonjwa wa akili wanaoonekana barabarani jijini Mwanza na maeneo mengine ya nchi wakiokota vitu majajalani wakitibiwa wanapona.

Akizungumza na Nipashe jana jijini hapa, Dk. Sembeye wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando, alisema wagonjwa hao wanapona wakitibiwa ingawa hawawezi kurudi kama walivyokuwa kabla ya kuugua.

Alisema kuna sababu nyingi ambazo zinachangia kuwapo wagonjwa wa akili ikiwamo kurithi, ugumu wa maisha, matumizi ya pombe, uvutaji bangi, madawa ya kulevya pamoja na ndoa kuvunjika.

Dk. Sembeye alifafanua kuwa ugonjwa wa afya ya akili kama haujakomaa kwa maana ya kuchukua muda mrefu, unapona.

Alisema Hospitali ya Bugando, kitengo cha magonjwa ya akili, wanapokea wagonjwa wa namna hiyo wapatao 100 kila wiki.

Kila siku wanahudumia wagonjwa wa akili wapatao 70 hadi 80 kwenye kliniki yao.

Sheria ya magonjwa ya afya akili ya mwaka 2008 inamtaka kila mtu kuwasaidia wagonjwa wa namna hiyo ikiwamo kuwapatia huduma.

"Kupitia sheria hiyo kila mtu ukiwemo hata wewe una wajibu wa kuwasaidia mgonjwa wa afya ya akili," alisema.

Akizungumzia tatizo la kuvunjika kwa ndoa linavyochangia wagonjwa wa afya ya akili, alisema inatokea ikiwa upande mmoja mke ama mume alikuwa anamtegemea katika maisha.

Alisema kama ndoa za namna hiyo zikivunjika mara nyingi upande mmoja hupata tatizo hilo.

Alisema mgonjwa wa namna hiyo akifikishwa kwao, wanatibu, lakini pia wanatafuta chanzo cha tatizo.

Alisema siku hizi wagonjwa wa afya ya akili wanazidi kuongezeka kutokana na ugumu wa maisha katika jamii.

Aliomba jamii kuwasaidia wagonjwa wa aina hiyo ili waweze kutibiwa na kupima badala ya kuweka mbele imani za kishirikiana kwamba wamelogwa.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## MWITO WA KUTOA MAONI

***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili. Pia inadhibiti Umeme na Maji Safi na Usafi wa Mazingira kwa kuhakikisha huduma zinazodhibitiwa zinapatikana kwa viwango vya ubora wa kutosha; kwa bei halisi; salama na kwa uhakika; na kwamba watoa huduma wanapata faida halali na stahiki kwenye vitega uchumi vyao.***

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/ Uraia | Aina ya Leseni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Cosmas Cornely Ndibalema T/A Mungu Bariki Oil Filling Station P.O. Box 561 Karagwe | Kijiji cha Kishoju Kata ya Kihanga Wilaya ya Karagwe, Mkoa wa Kagera. | Cosmas Cornely Ndibalema (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 2. | Jared Geofrey Komanya T/A Lake Tanganyika Oil Company - Buhigwe Petrol Station P.O. Box 58 Kasulu | Kiwanja Na 1 Kitalu "B" Eneo la Buhigwe Wilaya Buhigwe, Mkoa wa Kigoma. | Jared Geofrey Komanya (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 3. | Zubeda Hamisi Msakati Petrol Station- Kelema Maziwani, S.L.P 176, Kondoa, Dodwoma | Eneo la Kijiji cha Kelema Maziwani, Wilaya ya Chemba, Mkoa wa Dodoma | Zubeda Hamisi Msakati (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 4. | Zubeda Hamisi Msakati Petrol Station- Zajilwa, S.L.P 176, Kondoa, Dodoma | Eneo la Kijiji cha Zajilwa, Wilaya ya Chamwino, Mkoa wa Dodoma | Zubeda Hamisi Msakati (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 5. | Mwadembe Company Limited S.L.P 701 Njombe | Kijiji cha Ilongo, Kata ya Mahongole, , Wilaya ya Mbarali, Mkoa wa Mbeya | Leopord Dembe (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 6. | Engen Pugu Service Station S.L.P 78470 Dar es salaam | Kiwanja Na P1110, Eneo La Pugu Mwakanga, Manispaa Ya Ilala, Dar es salaam | Samuel Aggrey (Raia Wa Kenya) | Leseni Ya Kituo Cha Mafuta |
| 7. | Mbuyuni Filling Station S.L.P 141 Ruangwa | Kijiji Cha Mnero Miembeni, Wilaya Ya Nachingwea., Mkoa Wa Lindi | Bakari Mohammed Amanzi (Mtanzania) | Leseni Ya Kituo Cha Mafuta |
| 8. | Jonas N. Nyagawa – J.N Petrol Station S.L.P 40550 Dar es Salaam | Kiwanja Na. 125, Kitalu "E", Eneo la Kitwiru, Mkoa wa Iringa | Jonas Nyagawa (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 9. | Mount Meru Petroleum Ltd - Magugu S.L.P 7094 Arusha | Kiwanja Na. 1, Kitalu 'R', Eneo la Magugu, Wilaya ya Babati, Mkoa wa Manyara | Atul Mittal (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 10. | Southern Zone Gas Distributors Limited S.L.P 78 Mtwara | Kiwanja Na.36, Kitalu 10, Mtwara Mjini, Mkoa Wa Mtwara | Muzaffer Walli (Mtanzania) | Leseni Ya Usambazaji Gesi Ya Kupikia (LPG Superdealer) |
| 11. | Uchira Gas Supply S.L.P 304 Mtwara | Eneo La Vigaeni, Mtwara Mjini, Mkoa Wa Mtwara | Emmanuel Roman Mndeme (Mtanzania) | Leseni Ya Usambazaji Gesi Ya Kupikia (LPG Superdealer) |
| 12. | Nzuamukulu Magandi S.L.P 6215 Mbeya | Kiwanja Na. MBY-2, Kitalu "H", Barabara ya Sisimba, Jengo la NHC, Jiji la Mbeya | Nzuamukulu Magandi (Mtanzania) | Leseni Ya Usambazaji Gesi Ya Kupikia (LPG Superdealer) |
| 13. | Twiga Paper Products Limited S.L.P 20192 Dar es salaam | Kiwanja Na. 5858, Kitalu 58, Eneo La Chang'ombe , Wilaya Ya Temeke, Dar es salaam | Jebi Parekadan (Raia Wa India) | Leseni Ya Kituo Cha Mafuta Kwa Matumizi Binafsi |
| 14. | Modern Flexible Packaging Ltd S.L.P 9958 Dar es salaam | Kiwanja Na. 109-A, Eneo La Chang'ombe, Wilaya Ya Temeke, Mkoa Wa Dar es salaam | Imtiaz Haji (Mtanzania) | Leseni Ya Kituo Cha Mafuta Kwa Matumizi Binafsi |
| 15. | Yapi Merkezi Insaat Ve Sanayi Anonim Sirketi S.L.P 79317 Dar es salaam | Eneo La Soga, Wilaya Ya Kibaha, Mkoa Wa Pwani | Gokalp Kahraman (Raia Wa Uturuki) | Leseni Ya Kituo Cha Mafuta Kwa Matumizi Binafsi |
| 16. | Yapi Merkezi Insaat Ve Sanayi Anonim Sirketi S.L.P 79317 Dar es salaam | Eneo La Shaurimoyo, Wilaya Ya Ilala, Mkoa Wa Dar es salaam | Gokalp Kahraman (Raia Wa Uturuki) | Leseni Ya Kituo Cha Mafuta Kwa Matumizi Binafsi |
| 17. | Alliance One Tobacco Tanzania Limited S.L.P 1595 Morogoro | Kiwanja Na.2, Kingolwira, Wilaya Ya Morogoro, Mkoa Wa Morogoro | Simon John Peverelle (Raia Wa Malawi) | Leseni Ya Kituo Cha Mafuta Kwa Matumizi Binafsi |
| 18 | Happy Gas Enterprises S.L.P 17078 Dodoma | Kiwanja Na.2&3, Kitalu A, Kisasa B - Centre, Jijini Dodoma | Fred Nassoro Mbilinyi (Mtanzania) | Leseni Ya Usambazaji Gesi Ya Kupikia (LPG Superdealer) |

**Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.**

Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi; S.L.P 2857 Dodoma;
Simu +255 262329003-4; Nukushi:+255 262329005;Barua Pepe info@ewura.go.tz;
Tovuti: http://www.ewura.go.tz

Imetolewa na:

**MKURUGENZI MKUU**
**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Zinatakiwa hatua haraka kumaliza uhamiaji haramu

**MATUKIO** ya kukamatwa kwa raia wa kigeni hususan kutoka nchi za Afrika wakiingia nchini kinyume cha sheria na taratibu za uhamiaji, yamekuwa yakiongezeka kila uchao.

Ni mara chache kupita mwezi mmoja bila kusikia na kuona taarifa hizo kwenye vyombo vya habari, kiasi kwamba matukio hayo yamekuwa mambo ya kawaida.

Hatuna sababu ya kutaja mataifa ambayo wahamiaji wengi haramu wanatoka, lakini itoshe tu kusema kuwa nchi za pembe ya Afrika ndizo vinara, ingawa sababu hazijulikani.

Aidha, mahakama zetu kila uchao zimekuwa zikitoa hukumu zinazohusu kesi za uhamiaji haramu na kuwatia hatiani washtakiwa kisha kuwapa adhabu za kulipa faini na wengine vifungo.

Kutokana na hali hii, ni dhahiri kuna kila sababu kwa serikali kulichukulia jambo hili kwa umakini sambamba na kutafuta suluhisho la kudumu.

Tunasema hivyo kwa sababu mfululizo wa matukio haya unaweza kutoa picha kwamba mamlaka zetu haziwajibiki ipasavyo katika kulidhibiti.

Baadhi ya matukio ya karibuni ni vyombo vya ulinzi na usalama Mkoa wa Dar es Salaam kuwatia mbaroni wahamiaji raia wa kigeni 36 wakidaiwa kuwa wahamiaji haramu. Watu hao ni raia wa Ethiopia na Somalia.

Mkuu wa Mkoa huo, Aboubakar Kunenge, alisema jana kuwa watuhumiwa hao walikamatwa usiku wa kuamkia Novemba 15, mwaka huu kwenye fukwe za Mbweni wilayani Kinondoni, kati yao 30 wanatoka Ethiopia na sita wanatokea Somalia.

Juzi Idara ya Uhamiaji mkoani Dodoma ilitangaza kukamata watu 29 kwa madai ni wahamiaji haramu kutoka Ethiopia, Rwanda Uganda na Bangladesh, kwa kosa la kuingia nchini bila vibali.

Pia ilisema imewakamata Watanzania watano kwa tuhuma za kuwasafirisha wahamiaji hao, kwa kutumia usafiri wa bodaboda na gari aina ya Fuso. Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Dodoma, James Mwanjotile, alisema walikamatwa katika barabara kuu ya Iringa eneo la Mtera.

Alisema katika idadi hiyo, 15 ni Waethiopia, Wabangladesh wawili, Wanyarwanda 11 na mmoja kutoka Uganda.

Mikoa ya Dodoma na Pwani imekuwa ikiongoza kwa kukamatwa watuhumiwa wa uhamiaji haramu wanaoingia nchini kama mapito ya kuelekea mataifa mengine.

Tunafikiri kwamba katika mkakati wa kupambana na matukio haya, watu wote wanaojihusisha kuwahifadhi watu hao na kuwasafirisha nao wabanwe na sheria ipasavyo.


Wakibanwa, itakuwa vigumu wahamiaji haramu kupata hifadhi na msaada wa kuwawezesha kusafirishwa kuelekea katika nchi wanazokusudia kwenda.

Jambo linalotia matumaini, ni mpango uliotangazwa hivi karibuni na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali; kwamba watakaobainika kuhusika kuwasaidia wahamiaji haramu kwa kuwahifadhi au kuwasafirisha watadhibitiwa kupitia kushtakiwa pamoja na mali zilizohusika kama nyumba, magari kutaifishwa.

Hatua hiyo tunaamini kuwa itasaidia sana kuwadhibiti wahusika. Pia tunashauri Idara ya Uhamiaji kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama kuweka doria za kudumu pamoja na kuanzisha operesheni endelevu katika mikoa vinara kwa kupokea na kusafirisha wahamiaji haramu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace, MKURANGA

# Wakala wapandishao nauli stendi ya Ubungo wasifumbiwe macho

**UNAPOFIKA** katika Kituo Kikuu cha Mabasi Ubungo, jijini Dar es Salaam na unaingia katika stendi hiyo, utakutana na kinadada na kinakaka wanakukimbilia kwa kasi wakikuuliza 'safari ya wapi na wapi unakoenda?'.

Hao ni wakala wa kampuni za mabasi, wakiwasaidia kutafuta abiria wa mabasi mbalimbali.Sina shida sana na hao wakala, bali mtihani wangu uko katika namna kazi hiyo inavyofanyika.

Cha kushangaza, unakuta wakala ana tiketi na mpiga debe pia ana tiketi zake. Riziki inatafutwa katika mtindo huo wa maisha, mwisho wa siku kila mtu anatoka na chake alicholenga kimaslahi.

Hatukatai mtu kutafuta riziki. Ni kweli wapo watu ambao hawajui hata mabasi ya kampuni yanapaki wapi na pale yakofikia, wapo wapo tu!

Kituko nilichokiona katika stendi hiyo ya Ubungo, haina siku nyingi, bali kadhaa zilizopita, nikiwa katika safiri ya kwenda Dodoma. Usafiri ulikuwa unasumbua kutoka Dar es Salaam kwenda jijini Dodoma.

Inawezekana ni zao la kisichokuwa kinaendelea bungeni, maana ni ndani ya msimu mmoja, wabunge wateule walikuwa wanaenda kuapishwa, huku wengine wakitumia usafiri wa mabasi. Gari nyingi zilikuwa zimejaa.

> **Inawezekana ni zao la kisichokuwa kinaendelea bungeni, maana ni ndani ya msimu mmoja, wabunge wateule walikuwa wanaenda kuapishwa, huku wengine wakitumia usafiri wa mabasi. Gari nyingi zilikuwa zimejaa.**

Pamoja na kujaa kwa gari hizo, lakini kuna magari ambayo nauli zake zilikuwa zinachanganya abiria hasa mnapomuonyesha tiketi kwa kondakta.

Ni gari moja, kulikuwapo tiketii tiketi zilizouzwa, nikishuhudia wastani wa Sh. 17,000, wengine Sh. 22,000 wapo wa Sh. 23,000 na na hata Sh. 25,000.

Sasa ninaingia katika kujiuliza, inakuwaje katika gari moja kunakuwapo nauli tofauti katika gari ambalo hata vitk vya nani ni sawa katika mfumo maarufu wa 'two by two,'

Hata hivyo, inapotokea abiria anamuita kondakta akidai ufafanuzi wake, anajibu kwa kujiamini kabisa kwamba nauli sahihi ni shilingi 17,000 na ziada zingine anayejua ni mpiga debe aliyekatisha tiketi hiyo

Nikimrejea kondakta huyo, ni kwamba mpigadebe halipwi chochote, wakala nao wanajilipa. Sasa tunajiuliza, huyo mpigadebe anakuwa na nguvu gani kuliko wenye kampuni, hata wakafanya baadhi ya mambo kupitiliza?

Mtu akiangalia kwa kina kampuni zingine hazitumii wapiga debe na biashara inafanyika bila tatizo.

Ukiangalia kampuni zinazotoza nauli kubwa, nazo ndizo zinazotoa huduma za ziada safarini kama soda, maji, juisi na zinakuwa hata na maeneo ya kuchaji simu. Safari inakuwa ya raha na starehe.

Pia, kuna cha ziada kwamba mtu akifuatilia nauli to mwenendo wa kampuni za mabasi zenye nauli kubwa, ni ngumu kukuta malalamiko ya aina hiyo kutozwa nauli tofauti.

Magari ambayo unakuta nauli zake hazieleweki, ndizo hazina hata huduma za maboresho ndani ya safari, simulizi za soda na juisi.

# 36 mbaroni tuhuma za uhamiaji haramu

**Na Mwandishi Wetu**

VYOMBO vya ulinzi na usalama Mkoa wa Dar es Salaam vimewatia mbaroni wahamiaji raia wa kigeni 36 wakidaiwa kuwa wahamiaji haramu.

Watu hao ni raia wa Ethiopia na Somalia wanaodaiwa kuingia nchini kinyume na taratibu za uhamiaji.

Mkuu wa Mkoa huo, Aboubakar Kunenge, amewaonya Watanzania wanaoshiriki kuwahifadhi na kuwasafirisha kwa lengo la kupata fedha.

Kunenge amesema watuhumiwa hao walikamatwa usiku wa kuamkia Novemba 15, mwaka huu kwenye fukwe za Mbweni wilayani Kinondoni ambapo kati yao, 30 wanatoka Ethiopia na sita wanatokea Somalia.

Aidha, Kunenge alisema hata utaratibu unaotumika kusafirisha watu hao unakiuka sheria, haki na utu wa binadamu kwa sababu wengi wao wanafungiwa kwenye kontena zisizokuwa na hewa na wanapobainika kufariki dunia, maiti zao hutupwa kwenye vichaka.

Hata hivyo, Kunenge amevipongeza vyombo vya ulinzi na usalama kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya katika kukabiliana na matukio ya uhalifu na uvunjaji wa sheria.

Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Edmund Mroso, alisema kinachofuata baada ya watuhumiwa hao kukamatwa watafikishwa mahakamani.

Aidha, Mroso alisema wanaowasafirisha au kuwahifadhi wahamihaji haramu adhabu inaelekeza kifungo cha miaka 20, faini ya shilingi milioni 20 au vyote kwa pamoja ikiwamo kutaifisha mali zilizotumika.



Baadhi ya wahamiaji haramu 36 kutoka Ethiopia na Somalia wakiwa chini ya ulinzi wa vyombo vya ulinzi na usalama jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# UNICEF yateua watetezi vijana watatu

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Watoto la Kimataifa (UNICEF) Tanzania limeteua vijana watatu watakaokuwa watetezi kwa vijana wenzao.

Uteuzi umefanywa ikiwa ni wiki inayoelekea ya maadhimisho ya Siku ya Watoto Duniani kesho, ambayo ni siku ya kuchukua hatua ili kuwasaidia watoto.

UNICEF imesema vijana hao ambao ni watetezi mahiri katika jamii zao wamekuwa wakionyesha kuihamasisha jamii ipende kutoa haki za watoto.

Taarifa kwa vyombo ya habari iliyotolewa na Usia Ledama, mtaalamu wa mawasiliano, UNICEF Tanzania, imesema vijana hao wameonyesha lengo na nia ya kuleta mabadiliko kwa njia yoyote iwe ndogo au kubwa.

Watetezi hao vijana walioteuliwa na UNICEF Tanzania ni Abigail Chamungwana (Abby Chams), mwanafunzi wa shule ya sekondari, mwanamuziki, mwandishi wa nyimbo na mwanaharakati wa kijamii.

Abby amekuwa akifanya kazi na mashirika mengi yasiyo ya kiserikali kwa lengo la kuwapa wasichana wadogo uwezo wa kutetea haki zao na kusema bila woga.

Mtetezi wa pili ni Emmanuel Cosmas Msoka, mwanafunzi wa shule ya sekondari ambaye ni bingwa wa kutetea haki za watoto.

Emmanuel ni makamu mwenyekiti wa Halmashauri ya Vijana mkoani Arusha, na wakati shule zimefungwa kwa sababu ya COVID-19, alitumia muda mwingi kusaidia watoto katika kituo cha watoto yatima huko Arusha, wakaendelea na masomo wakati pia akiwafundisha na kuwaongoza kuchukua hatua za tahadhari za kiafya zilizopendekezwa kukabiliana na Corona.

Mtetezi wa tatu ni Raphael Denis ambaye kwa sasa yupo chuo kikuu, na amekuwa akitetea harakati zinazojumuisha watoto na vijana.

Raphael ana uzoefu wa miaka saba ya uongozi katika Baraza la Vijana la kitaifa, ambapo amekuwa mstari wa mbele katika kazi ya utetezi kumaliza ukatili dhidi ya watoto.

Anatamani kuendelea kupigania haki ya kibinadamu, na pia ni sehemu ya mpango wa mtandao wa UNICEF Tanzania ambao unalenga kutangaza maendeleo na mafanikio za vijana.

Usia alisema watetezi hao watatu wa vijana watajiunga na timu ya kimataifa ya watetezi vijana wa UNICEF na baadhi yao watashirikiana na mtetezi mzoefu wa UNICEF Millie Bobby Brown.

"Ulimwenguni kote, watoto na vijana wanakuja na suluhisho la ubunifu kutatua shida za leo, pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa na ujifunzaji wa mbali wakati wa janga la corona. Nimefurahi kuungana na watetezi wengine kuinua sauti zetu kwa maendeleo ya vijana," alisema Brown.

UNICEF Tanzania inashirikiana na watoto na vijana kujenga uwezo wa vijana kuwa mabingwa na kuleta mabadiliko.

Mwaka 2019, wakisaidiwa na UNICEF, vijana na watoto wa Tanzania walitengeneza ajenda yao ya 'Watoto na Vijana', ambayo ilizinduliwa katika maadhimisho ya Siku ya Watoto Duniani 2019 na kuelezea masuala ya kipaumbele yaliyotambuliwa na wao wenyewe.

Watetezi wa vijana wametambuliwa baada ya mchakato wa kuchagua kwa uangalifu kutambua talanta inayoahidi ambayo inaweza kuhamasisha mabadiliko katika jamii.

"Kati ya watu wanaokadiriwa kuwa milioni 60 Tanzania, zaidi ya asilimia 50 wako chini ya miaka 18 na zaidi ya asilimia 70 wako chini ya miaka 30," alisema Mwakilishi wa UNICEF Tanzania, Shalini Bahuguna.

Wakati wa maadhimisho ya Siku ya Watoto Duniani, UNICEF inahimiza kila mtu asimame na watoto na vijana wanapofanya kazi kuelekea maisha bora.

# Serikali yashauriwa kutenga bajeti kukuza elimu jumuishi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeshauriwa kutenga bajeti ya kutosha, ili kuwezesha elimu jumuishi nchini kusaidia watoto wenye ulemavu na wale kutoka jamii za wafugaji kupata elimu bila kikwazo.

Mkurugenzi wa Kituo cha Habari kuhusu Ulemavu (ICD), Fredrick Mkatambo, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mradi wa elimu jumuishi utakaotekelezwa Wilaya ya Bahi na Jiji la Dodoma.

Mkatambo alisema serikali kuwekeza fedha katika elimu jumuishi, kutasaidia kuondoa kero mbalimbali ambazo zimekuwa zikikwamisha watoto wenye ulemavu kupata haki ya msingi na kuleta mabadiliko katika sekta ya elimu nchini.

Alisema hivi sasa elimu jumuishi inakabiliwa na kero mbalimbali ikiwamo miundombinu isiyo rafiki kwa watoto wenye mahitaji maalum.

"Elimu jumuishi si tu kuchanganya watoto wenye ulemavu bali kuhakikisha changamoto zote zilizopo zinafanyiwa kazi kama vile miundombinu ya madarasa, lakini walimu kwa ajili ya kuwafundisha watoto hawa wenye mahitaji maalum," alisema Mkatambo.

Pia alisema mradi huo kwa miaka kadhaa umekuwa ukitekelezwa katika mikoa ya Katavi, Sumbawanga na Rukwa. Kati ya shughuli wanazozifanya ni kukarabati miundombinu ya shule.

"Tumekuwa tukikarabati miundombinu ya shule kama vile uwekaji wa ngazi msererereko kwa ajili ya watu wenye ulemavu na kutoa elimu kwa walimu namna ya kufundisha hawa watoto," alisema.

Kadhalika, alisema baadhi ya kero ambazo wamekuwa wakikumbana nazo wakati wa utekelezaji wa mradi huo kwenye mikoa hiyo ni shule nyingi kukosa miundombinu rafiki kwa ajili ya walemavu.

Mkatambo aliiomba serikali kuweka sera maalum kwa ajili ya elimu jumuishi na kutoa maelekezo katika halmashauri zote kuwa na mwongozo wa aina moja ya majengo ya madarasa.

Lengo la mradi huo, alisema ni kuhakikisha serikali inaiga wanacho kifanya katika suala la ukarabati wa majengo ya shule.

"Hivi sasa shule nyingi hazina ngazi msererreko, milango midogo watoto walemavu wanaotumia viti vya magurudumu hawezi kupita lakini madirisha madogo ni shida kwa watoto wenye uoni hafifu, haya yote yanahitaji serikali kuweka mkakati wa kuyafanyia kazi," alisema.

Pia alisema kuwekeza katika elimu jumuishi kutasaidia kuondoa tatizo la watoto kumaliza darasa la saba wakiwa hawajui kusoma na kuandika.

Alisema watoto wanamaliza darasa la saba wakiwa hawajui kusoma na kuandika kutokana na walimu kukosa stadi muhimu kwa ajili ya kufundishia na kuamua kuwatelekeza.

## Wapewa somo kuhusu kujiajiri

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

VIJANA wanaohitimu katika vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi (VETA), wameshauriwa kutumia ujuzi walionao kujiajiri na kuacha kutegemea ajira kutoka serikalini ambazo ni chache.

Wametakiwa kutumia elimu wanayoipata kwa kufungua vituo vya urekebishaji wa magari, umeme na ufundi cherehani.

Mwenyekiti wa Parokia ya Kahama Mjini, Edward Kinunga, alisema hayo juzi wakati wa mahafali 17 ya Chuo cha Ufundi cha St. Francis De-Sales Mwakata. Alisema kufanya hivyo ni kuendelea kupambana na tatizo la ajira.

Alisema kuhitimu chuo cha ufundi na kukaa nyumbani kutegemea ajira kutoka serikalini ni kupoteza muda na kushindwa kufanya shughuli za kiuchumi kwa kutumia ujuzi uliopata chuoni, hivyo wanatakiwa kufungua vituo vya ufundi kulingana na fani walizosomea.

"Kumbukeni hamkuwa chuoni kukaa tu bali mlikuwa mkipata elimu au kuelimika kwa kupata ujuzi ambayo ndio mkombozi wako katika maisha ya baadaye. Shule zetu za msingi zinatoa vijana kila mwaka na wanakosa nafasi kama hii mliyoipata. Nendeni mkatumie ujuzi wenu kuwaelimika, alisema," alisema Kinunga.

Naye Mkuu wa Chuo hicho, Padri Thomas Njeru, alisema mbali na kutoa ujuzi mbalimbali kwa vijana, bado wamekuwa wakiwapatia elimu ya namna ya kujiajiri kwa kutumia ujuzi wao, ili kuwaondolea dhana ya kuendelea kutegemea kazi kutoka serikalini.

Pia aliyashukuru mashirika yasiyo ya kiserikali yanayoshirikiana na chuo hicho kuwaelimisha vijana waliohitimu elimu ya msingi na sekondari na kushindwa kuendelea na masomo. Mashirika hayo ni PACT Tanzania, TADEPA, Msalaba Mwekundu, KIHOWEDE na wazazi.

Awali, akisoma risala kwa mgeni rasmi, Adela Ramadhani, mwanafunzi wa chuo hicho, alisema wanafunzi 190 wa ujuzi mbalimbali ikiwamo ujuzi wa umeme, magari, batiki, udereva na ushonaji walihitimu mafunzo hayo.

Hata hivyo, Ramadhani alisema chuo hicho kinakabiliwa na ukosefu wa maji ya uhakika, vifaa vya kujifunzia, viti, meza na miundombinu rafiki ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ambao wako zaidi ya watano.

Mratibu wa Mafunzo wa Chuo hicho, Charles Maganga, alisema licha ya kuwa na ukosefu wa maji ya kutosha, bado wanatumia magari kusomba maji na kuendelea kuwafundisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwa kutumia uzoefu.

# Waajiriwa waandaliwa mafunzo kustaafu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC), inakusudia kutoa mafunzo kwa waajiriwa wapya na walioko kazini kuwajengea uwezo wa kuendesha miradi mbalimbali itakayosaidia baada ya kustaafu.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Aloyce Nzuki, alisema hayo juzi wakati akifungua mafunzo ya siku 28 kwa watumishi wa idara mbalimbali za wizara hiyo ambao wanatarajia kustaafu katika utumishi wa umma.

"Binafsi ninaona sasa kuna umuhimu wa kutoa mafunzo tangu pale waajiriwa wapya wanaoingia ofisini wajifunze kufanya biashara, kutunza hesabu za kibiashara, uwekezaji baada ya kuchukua mikopo inayolipika ili wapate uzoefu badala ya kusubiri wakati wa kukaribia kustaafu," alisema Dk. Nzuki.

Alisema kwa sasa ni muhimu kwa waajiriwa wapya wakafundishwa namna ya kufanya biashara, ili wawe na uzoefu endelevu kwenye biashara hata wakistaafu wanakuwa wanajua namna ya uendeshaji wa biashara.

Dk. Nzuki pia aliwataka watumishi wanaotarajia kustaafu kuepuka visababishi vya msongo wa mawazo kwa kuwa madhara yake ni makubwa kiafya na badala yake watumie mbinu za kukabiliana na hali hiyo.

Mratibu wa Mafunzo hayo kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma, Judith Mnguli, alisema kustaafu kazi si kustaafu maisha, hivyo kupitia mafunzo hayo, wanawapatia mbinu mbalimbali za kuzitumia za kiuchumi kwa ajili ya kujitegemea baada ya kustaafu.

Alisema mafunzo hayo ni ya kuandika andiko la mpango kazi wa miradi, uwekezaji kwenye biashara na aina ya miradi ya kuwekeza baada ya kustaafu utumishi wa umma.

Mnguli alisema eneo la uwekezaji ni lile unalolenga kuwa na thamani, ujuzi wa uendeshaji wa miradi na uanzishaji wa miradi iliyorafiki yenye kuleta faida kwao.

Mratibu huyo alisema suala la mafunzo kwa waajiri wapya litafikishwa katika uongozi wa chuo hicho, ili kuingizwa kwenye mpango ya chuo kwa ajili ya kuona namna ya utekelezaji wake.

Naye Ofisa Wanyamapori Mkuu, Charles Mvungi, akizungumza kwa niaba ya wenzake, alimpongeza Katibu Mkuu kwa kuridhia kupewa mafunzo hayo.

Pia aliwasilisha ombi la kuharakishiwa mafao yao ya kustaafu ili kuzitumia fedha kufanya shughuli za biashara na kilimo, jambo litakalowaondolea msongo wa mawazo.



Mkurugenzi Mkuu wa Total Tanzania, Jean-Francois Schoepp, akifungua boneti ya gari, wakati wa uzinduzi wa wiki ya huduma kwa wateja ya kampuni hiyo kwa mwaka huu, katika kituo cha mafuta cha Total Africana, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaume walia makali usawa kijinsia

**Na Christina Haule,** MOROGORO

BAADHI ya wanaume katika vijiji 10 vya wilaya za Morogoro, Mvomero na Kilosa mkoani Morogoro, wameilalamikia serikali kwa kuhimiza mgawanyo wa majukumu uende sawa kijinsia na kufikia asilimia 50 kwa 50 ifikapo mwaka 2035.

Kwa mujibu wa malalamiko ya wanaume hao, hatua hiyo inaingilia masuala ya mila na hali zao kimaisha.

Mwezeshaji wa mada ya jinsia kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Prof. John Jeckoniah, alisema hayo jana wakati akitoa taarifa ya matokeo ya awali ya utafiti uliofanywa na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) kwa kushirikiana na Mtandao wa Usimamizi wa Misitu ya Kijamii Tanzania (MJUMITA).

Utafiti huo pia umejumuisha Shirika la Kuendeleza Nishati ya Asili Tanzania (TaTEDO) kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Uswisi (SwissAID) kwa wadau wa misitu uliofanyika mjini hapa.

Prof. Jeckoniah alisema katika kutekeleza mradi wa kuleta mageuzi katika sekta ya mkaa Tanzania (TTCS) maarufu kama mkaa endelevu, mashirika hayo yalitoa elimu ya masuala ya kijinsia na kuwafanya baadhi ya wanawake kushiriki katika shughuli za Uhifadhi na Usimamizi wa Misitu Kijamii (USMJ), hivyo kuona faida ya msitu.

Alisema suala la kutekeleza mradi wa mkaa endelevu na mazao mengine ya misitu lilileta mafanikio kiuchumi kwa baadhi ya wanawake na kufanya kuzuka kwa changamoto mbalimbali kwenye ndoa zao, huku wasiokuwa na ndoa kwao hilo kutokuwa kikwazo.

Pia alisema hali ya mabadiliko ya kiuchumi kwa wanawake imewafanya wanaume waliowengi kukasirishwa na ufuatiliaji na usimamizi wa masuala ya uzalishaji wa mazao ya misitu kijinsia kwa madai kuwa suala la mitazamo ya kijinsia limeharibu mila na desturi zao na kuwafanya kudharaulika.

Alisema kukua kiuchumi kwa wanawake pia kulisababisha vipigo kwa wanawake kutoka kwa waume zao na wanaume kutoka kwa wake zao, jambo ambalo limezua migogoro mingi na kusababisha baadhi ya ndoa kuvunjika.

Prof. Jeckoniah alisema pia katika utafiti wamebaini kuwa katika maeneo mengi bado wanaamini kuwa kazi za USMJ ni za wanaume kutokana na kuwa nyingi ya kazi hizo zinahitaji nguvu na akili na kusahau kuwa wako baadhi ya wanawake wenye uwezo huo huku wanawake wakilalamikia kuendelezwa mfumo dume na kusababisha baadhi yao kukatazwa kuendelea kufanya shughuli za USMJ.

Kutokana na matokeo hayo ya utafiti, aliishauri jamii kutambua kuwa uwiano wa kijinsia unapaswa kuzingatiwa ili kuleta maendeleo chanya katika nchi yoyote duniani na kusisitiza kuwa elimu ya masuala ya kijinsia inapaswa kutolewa kwa jamii ili kuleta mabadiliko yanayotakiwa.

Alisema kutokuwapo kwa uwiano wa kijinsia kuna nafasi kubwa ya kuathiri mfumo mzima wa kukua kwa uchumi wa nchi yoyote na kwamba masuala ya kijinsia yanapaswa kutekelezwa katika kila hatua ya maisha ya mwanadamu kwa sasa.

## NSSF yafikishia huduma wananchi wa kawaida

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), limeendelea kusogeza karibu huduma kwa wanachama wake katika kuhakikisha wana maisha bora kabla na baada ya kustaafu.

Akizungumza hivi karibuni mwanachama wa NSSF, Samwel Jacob, alisema shirika hilo limekuwa la wananchi wengi katika sekta binafsi wakiwamo wachimbaji madini, kwani linatoa huduma za hifadhi ya jamii na kushughulikia masuala mbalimbali ya wanachama wao.

Alisema anafurahia huduma mpya zilizoboreshwa na shirika hilo zikiwamo za kupata taarifa mbalimbali za michango yake kupitia simu ya mkononi na kompyuta mpakato bila ya kulazimika kufika katika ofisi za NSSF.

"Huduma zinazotolewa na NSSF ni nzuri kwani zinamrahisishia mwanachama kupata taarifa sahihi pamoja na kupunguza muda wa kuhitaji taarifa hizo ofisini," alisema.

Akizungumzia namna shirika lilivyoboresha mifumo ya uandikishaji wanachama, Ofisa Matekelezo NSSF mkoani Geita, Jackson Mbengo, alisema mifumo ya uandikishaji wanachama na sasa wanatumia namba ya kitambulisho cha Taifa (NIDA) kuandikisha wanachama, jambo ambalo limekuwa rahisi.

"Mwanachama anapokuwa amejaza fomu yetu akawa ameandika namba yake ya NIDA hana haja tena ya kufika kwenye ofisi zetu, ili aweze kuandikishwa kama ilivyokuwa zamani," alifafanua.

Alisema utaratibu huo umerahisisha shughuli za shirika la kuandikisha wanachama, na kutoa wito kwa waajiri waliopo katika sekta binafsi kuhakikishe wafanyakazi wao wanaandikishwa NSSF, ili waweze kuwekewa mafao yao ya baadaye.

Ili mwanachama aweze kunufaika na mafao mbalimbali yanayotolewa na NSSF ni muhimu kuwasilisha michango yake kwa wakati kama anavyoyeleza, Ibrahim Chombenga ambaye ni Ofisa Matekelezo NSSF mkoani Geita.

Aidha, alisema miongoni mwa kazi wanazofanya ni kusajili wanachama na kufuatilia michango kwa waajiri ambayo ni asilimia 10 kutoka kwa mwanachama na asilimia 10 kutoka kwa mwajiri, lengo ni kuhakikisha wanachama wananufaika na mafao yanayotolewa na NSSF.

Naye Ofisa Matekelezo kwa sekta isiyo rasmi mkoani humo, Blandina Gama, alisema wanatoa elimu kwa wanachama waliopo katika sekta isiyo rasmi kama wavuvi, wafugaji, wachimbaji wadogo ambao wanawaandikisha kwa kutumia kitambulisho cha NIDA.

Alibainisha kuwa mwanachama anayejichangia kwa hiari ulipaji wake michango ni rahisi zaidi kwa sababu anapatiwa namba ya kumbukumbu ambayo ataitumia kulipia michango yake na kiwango cha chini ni shilingi 20,000.

# Ofisa LATRA aliyetishia kwa panga asimamishwa

**Na Edwin Mhagama**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), imemsimamisha kazi ofisa leseni wa mamlaka hiyo mkoani Lindi, kwa tuhuma za matumizi ya nguvu kupita kiasi dhidi ya dereva wa gari la mizigo.

Tukio hilo lililosambaa kwenye mitandao ya kijamii likimwonyesha ofisa huyo aligombana na dereva, huku akizuiwa na askari polisi, na baadaye alichukua silaha (panga) kwenye gari lake akitaka kumdhuru dereva huyo na kutaka aandikiwe faini ya Sh. 500,000.


Akizungunza na waandishi wa habari jana, jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Gilliard Ngewe, alisema mamlaka hiyo imesikitishwa na kitendo hicho kwa kuwa kinakiuka misingi ya utumishi.

"Kufuatia tukio hilo, uongozi wa mamlaka ulimsimamisha kazi ofisa huyo na hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria dhidi yake zinaendelea kuchukuliwa, hatua ya kumsimamisha kazi imechukuliwa kwa mujibu wa kanuni za utumishi wa umma za mwaka 2003," alisema Ngewe.

Aidha, alisema mara kwa mara imetoa mafunzo ya kimaadili ya utumishi wa umma pamoja na kufuatilia utendaji kazi wa watumishi wake kwa lengo la kuhakikisha wanafanyakazi kwa mujibu wa sheria na kanuni.

Mkurugenzi huyo alikemea tabia hiyo na kuwaonya watumishi wengine.

"Mamlaka inakemea vikali kitendo cha mtumishi huyo na watumishi wengine wenye nia ya kufanya tukio kama lile, waache mara moja ni kinyume cha sheria na hakiendani na mienendo ya watumishi wa LATRA, mamlaka itaendelea kuhakikisha wafanyakazi wake wanafuata sheria , miongozo na taratibu zilizopo katika kudhibiti sekta ya usafirishaji ardhini."



Wanafunzi wa Chuo cha Ufundi St. Francis De-Sales Mwakata kilichopo Kata ya Mwakata, Halmashauri ya Msalala, mkoani Shinyanga, wakionyesha ujuzi wao wa kufunga soketi ya kuwasha mashine ya kusaga nafaka wakati wa mahafali ya 17 ya chuo hicho, jana. **PICHA: SHABAN NJIA**.

# Serikali yaahidi ushirikiano kuhudumia wenye usonji

**Na Richard Makore,** MWANZA

SERIKALI imeahidi kushirikiana na kufanya kazi na wadau waliojitolea kuwahudumia watoto wenye matatizo ya mfumo wa fahamu (usonji).

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Nyamagani jijini Mwanza, Dk. Phillis Nyimbi, katika hafla ya kugawa misaada kwa watoto wenye usonji.

Hafla hiyo iliandaliwa na Shirika la Living Together Autistic Foundation (LI-TAFO) kwa lengo la kukusanya fedha za ujenzi wa kituo cha kuwahudumia watoto wenye usonji.

Alisema jamii inatakiwa kuwa pamoja na kuwahudumia watoto wa namna hiyo na kwamba serikali kwa muda wote imekuwa mstari wa mbele kuboresha huduma za afya nchi nzima.

Aliwaomba wadau mbalimbali kuguswa na matatizo ya watoto hao na kuitaka jamii kuachana na imani za kushirikina na kuona shida hiyo inatokana na kulogwa.

Daktari bingwa wa mishipa ya fahamu wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando, Yusuph Jamnagerwalla, alisema tatizo la usonji ni kubwa.

Alisema kila wiki wanapokea watoto wenye tatizo hilo na kwamba changamoto iliyopo wazazi wanachoka kusafiri umbali mrefu kutafuta huduma ya watoto hao.

Aliwataka madaktari kuwafanyia uchunguzi ili kubaini tatizo hilo, na kwamba hawajabaini ugonjwa huo unasababishwa na nini.

"Hatujui sababu ya usonji ni nini, licha ya wataalamu kufanya utafiti ili kubaini chanzo cha tatizo hilo," alisema.

Aliongeza kuwa kuna uhaba wa wataalamu kwa ajili ya kutibu watoto hao, na kuomba kuanzishwa kitengo maalum kwa ajili ya kutoa huduma hiyo.

Alisema kwa sasa wanachanganya watoto wenye usonji na wenye matatizo ya utindio wa ubongo, jambo ambalo siyo sahihi.

Mkurugenzi wa LI- TAFO, Shangwe Mgaya, alisema wanawake walizozaa watoto wenye usonji wanakumbana na changamoto nyingi.

Alitaja changamoto hizo ni pamoja na ugumu wa kuwalea na kwamba jamii bado haijakubali kuwapo tatizo hilo.

Alifafanua kwamba watoto wenye usonji, wanashindwa kuwasiliana, kuchangamana pamoja na kushindwa kuzoea mazingira mapya.

# Mbaroni tuhuma kulawiti mtoto

**Na Said Hamdani,** LINDI

JESHI la Polisi Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi, linamshikilia kwa mahojiano mkazi wa Kijiji cha Naunambe, Kata ya Mbekenyera, Ally Chikukula (23) kwa tuhuma za kulawiti mtoto .

Hayo yameelezwa na Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Foka Dinya na kuwa mtuhumiwa alikamatwa Novemba 15, mwaka huu, katika Kijiji cha Naunambe akidaiwa kumlawiti mtoto mwenye umri wa miaka sita (jina limehifadhiwa).

Dinya alisema Chikukula alikamatwa na wananchi baada ya mtoto huyo kupiga kelele za kuomba msaada kutoka kwa majirani, na kwamba walipofika walimkuta mtuhumiwa akitekeleza unyama huo.

Alisema baada ya wananchi kumkamata mtuhumiwa huyo walimfikisha Polisi kisha kupelekwa Kituo cha Afya Kata ya Mbekenyela na kubainika kuingiliwa.

Dinya amesema mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kujibu shtaka linalomkabili wakati wowote baada ya kukamilika kwa taratibu.



Meneja chapa msaidizi wa Benki ya NCBA Tanzania, Nasikiwa Berya (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Dk. Deborah Maufi wa Babymoon Care ya Uholanzi, kuhusu jinsi ya kumwandaa mtoto aliyezaliwa njiti awe katika hali ya usalama, afya na uangalizi mzuri, ili aweze kukua kwa wakati, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto Njiti Duniani kwenye viwanja vya Hospitali ya Taifa Muhimbili, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU** .

# H/shauri yakopesha vikundi mil. 290/-

**Na Vincent Tiganya,** TABORA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora, imetoa vifaa vya usafiri na mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 290 kwa vikundi mbalimbali ikiwa ni sehemu ya asilimia 10 ya mapato yake ya ndani.

Mikopo hiyo ilikabidhiwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, kwa niaba ya uongozi wa halmashauri hiyo.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi mikopo hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua, Jerry Mwaga, alisema kati ya fedha hizo, shilingi milioni 156 zimetolewa kwa vikundi 17 vya vijana na shilingi 119 zimetolewa kwa vikundi 23 vya wanawake na shilingi milioni 15 zimetolewa kwa vikundi vitano vya watu wenye ulemavu.

Alisema kati ya fedha zilizotolewa kwa vikundi vya vijana, shilingi milioni 72 zimetumika kununua pikipiki 30 ambazo zimetolewa kwa vikundi vya bodaboda Kata za Ushokola, Usinge na Ichemba.

Mwaga alisema Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua imeendelea kutenga asilimia kumi ya mapato ya ndani kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na walemavu vilivyosajiliwa.

Alisema kuanzia mwaka wa fedha wa 2014/15 hadi 2020/21 wameshakopesha jumla ya shilingi bilioni 1.4 kwa vikundi 330.

Mwaga alisema vikundi vya vijana 128 vimekopeshwa jumla ya shilingi 772.4, wanawake vikundi 177 vimekopeshwa milioni 605.3 na vikundi 25 vya watu wenye ulemavu vimekopeshwa shilingi milioni 71.5.

Aidha, alisema wanaendelea kufuatilia deni la shilingi bilioni 1 ambazo ni fedha zilizokopeshwa kwa vikundi na haijarejeshwa na wakopeshwaji.

Dk. Sengati alizitaka halmashauri nyingine mfano wa Kaliua katika utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa ajili ya makundi hayo.

# Walimu wasaidia wanafunzi wenye uhitaji maalum

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

KIKUNDI cha walimu wazalendo wa shule za msingi Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, wametoa msaada wa vifaa mbalimbali vitakavyosaidia kujengwa kwa choo kwa ajili ya wanafunzi wenye uhitaji maalum katika Shule ya Msingi Vikundi.

Msaada huo unajumuisha fedha taslimu shilingi 400,000, lori moja la mchanga na matofali 1,000.

Akikabidhi msaada huo, kiongozi wa kikundi hicho, ambaye ni mwalimu wa Shule ya Msingi Ngunguti, Hamis Ndome, alisema lengo la kutoa msaada huo ni kuwawezesha watoto wenye uhitaji kupata choo ambacho kitawawezesha kukitumia bila woga.

"Tujenge utamaduni tunapobarikiwa chochote, tuwakumbuke na wale walio na uhitaji maalum," alisema.

Aliwataka walimu wajenge utamaduni wa kujitolea badala ya kulalamika.

Mwalimu Bakari Jili alisema utamaduni waliojiwekea ni kutumia stahiki zao ili kusaidia makundi mbalimbali ya kijamii ikiwamo kuthibitisha uzalendo wao kwa serikali na kwa wananchi.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mwanambaya, Priscila Mtenga, alisema wameamua kuwasaidia wanafunzi wenye uhitaji maalumu ili nao wapate elimu wakiwa katika sehemu salama ya choo.

## Shule zakamilika kupokea wanafunzi kidato cha 1

**Sabato Kasika**

JUMLA ya shule mpya tano za sekondari, Wilaya ya Musoma mkoani Mara, zinatarajia kuanza kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza mwakami ikiwa ni jitihada za wilaya kuboresha elimu.

Shule hizo ni Bukwaya, Kigera, Nyasaungu, Ifulifu na Seka, ambazo sasa ujenzi wake uko hatua za mwisho, kwa ajili ya kupokea wanafunzi hao ambao walifanya mtihani wa taifa wa darasa la saba mwaka huu.

Ofisa Elimu Sekondari wa wilaya hiyo, Majidu Karugendo, alibainisha hayo alipokuwa akizungumza na gazeti hili kuhusu mikakati ya inayoendelea wilayani humo ya kuboresha elimu.

"Mbali na hizo, tunatarajia kujenga sekondari nyingine tano za kata kuanzia mwaka kesho ambazo ni Etaro, Makojo, Mugango, Suguti na Tegeruka ikiwa ni mwendelezo wa kuboresha elimu wilayani mwetu," alisema Karugendo.

Alisema, wakazi wa wilaya hiyo wanaongozwa na kaulimbiu ya 'Elimu Kwanza', ambayo imewawezesha kujitolea katika ujenzi wa shule za sekondari kwa ajili ya watoto wao.

"Kwa sasa wilaya yetu ina vijiji 68, kata 21 na shule sekondari 20 za kata na mbili za binafsi, lakini wananchi wanaendelea kushirikiana na serikali katika jitihada za kuongeza sekondari nyingine," alisema.

Karugendo alifafanua kuwa, miaka mitano ijayo, wanatarajia kuongoza shule za kidato cha sita kutoka mbili zilizopo sasa hadi kufikia sita, na kwamba hilo litawezekana kwa vile wamedhamiria.

Naye Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo, alisema yeye ni miongoni mwa wadau wa elimu na kwamba amekuwa akitoa michango mbalimbali kwa ajili ya kuboresha elimu.

"Kwa mfano, nimetoa mifuko 150 ya saruji na mingine 100 kwa Fedha za Mfuko wa Jimbo, mabati 108, na huo ni mchango wangu kwa Kigera Sekondari, lakini nimeshachangia sekondari zote," Prof. Muhongo alisema.



Ukurasa 12

**Umma wafunguka macho ukatili jinsia unavyowamaliza afya zao**



Ukurasa 14

**Wazalishaji Coca-Cola rasmi kusafisha fukwe unaochafuliwa na utitiri plastiki**

# Majeruhi wa ajali gari kupinduka mara 3 alivyopewa maisha mapya

- Hajiwezi...'yaleyale' arejeshewa ukapera
- Mwanasheria trafiki aanika hali kitaifa

**Na Beatrice Shayo**

ALHAMISI wiki iliyopita, safu hii ilikuwa na mkasa wa majeruhi wa ajali kuanguka ghorofani. Leo ni simulizi ya mkasa unaofanana, safari hii ajali ya barabarani. Fuatilia:

"Nilivyopata ajali huduma ya kwanza ilikuwa ni kikwazo cha mimi kupata madhara makubwa katika mwili wangu, anayeniokoa hana uelewa wa kumsaidia mtu aliyepata ajali wananivuta kumbe wanazidi kuniongezea tatizo".

Ni maneno ya Abdulaziz Shamba. Ilikuwa mwaka 2003 alipokuwa safarini kulekea mkoani Tanga, gari lake ilipinduka mara tatu na akapata madhara shingoni na kuvunjika.

"Huduma ya kwanza pale tulipopata ajali likuwa shida, watu walikuwa wanafikiria kuiba na sio kutusaidia. Aliyekuwa anahangaika ni dereva wangu, mimi nilikuwa nimefunga mkanda gari ilivyopinduka ukawa unanibana kwenye shingo.

"Kutokuelewa kwa dereva, alikuja kunivuta akachangia hali yangu kuwa mbaya kiasi hiki, hakuwa na elimu ya kumsaidia aliyepata ajali," anasema Shamba.

Shamba, ambaye ni Katibu Mkuu wa Chama cha Watu Walioumia Uti wa Mgongo, anasimulia eneo alilopata ajali lilikuwa kijijini na hapakuwapo huduma za afya jirani.



Abdulaziz Shamba, majeruhi wa ajali ya barabarani, akisimulia kilichomsibu. **PICHA: BEATRICE SHAYO.**

Anasema licha ya gari kuwa na vifaa vipya, zikiwamo matairi, anahisi chanzo kikuu cha ajali kilikuwa mwendo kasi. Hata hivyo, hakufafanua.

"Basi...lilinipakia na kunipeleka kituo cha afya, nilivyofika pale mwanajeshi mmoja akiwa eneo hilo aliniona, akasema kwa hali yake apatiwe rufaa apelekwe Hospitali ya Muhimbili.

"Pale kijijini hapakuwapo gari la kubebea wagonjwa, bahati nzuri fahamu zilivyonijia, niliulizwa namba ya simu nikataja namba ya mtu wa ofisini Tanga," anaeleza Shamba, wakati huo akiwa meneja katika kampuni ya mafuta.

Anaeleza, mfanyakazi mwenzake aliyekuwapo Tanga aliwasiliana na Hospitali ya Rufani Bombo, alikosa gari kwa sababu iliyokuwapo haikuwa na uwezo kusafiri hadi Dar es Salaam.

**SAFARI MUHIMBILI**

"Ilikuja kupatikana Hiace (basi dogo) ya mtu binafsi wakatoa viti wakaweka godoro, wakatupakia kutuleta. Nimepata ajali saa tisa alasiri Muhimbili tumefika saa sita usiku," anaeleza.

Shamba anasema Tasisis ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI) ilikuwa haijaanza matibabu ya shingo, hivyo alikaa wodini kwa siku 14 madaktari wakijadiliana namna ya kumsaidia.

Anasimulia kipindi hicho alipatiwa dawa za kupunguza maumivu na baada ya siku 14, ukafikiwa uamuzi apelekwe nchini Afrika Kusini kwa matibabu zaidi na alipofika huko, alijulishwa amecheleweshwa matibabu kwenye huduma za awali.

"Nimeambiwa huduma ya kwanza nilitakiwa kutenganishwa sehemu niliyoumia ambayo sikupatiwa hadi nilivyofika Afrika Kusini. Hapa nilivalishwa ya shingoni (neel cap) hawajatenganisha ile mishipa ndio maana nimepata madhara zaidi," anasema.

Shamba, wakati huo alikuwa Katibu Mkuu wa Klabu ya Moro United na ndoto yake ilikuwa kufanya kazi u kocha wa soka, fani aliyosomea nchini Sweden na hadi anapata ajali, alikuwa na siku 12 tangu kurejea nchini, ndoto hizo zikatoweka.

Anasmulia kiafya, walimshauri na kumsaidia kurudia maisha ya kawaida, ingawa hajaweza kutekeleza vilivyo, kutokana na ulemavu wa sasa.

Anadokeza shida inayomkabili sasa, akieleza:"Ofisi ilikuwa inakutibia, wanakutegemea upone urudi ofisini. Wanaona muda unazidi kwenda hauponi na wao walifika wakati wakachoka na kukata tamaa kunitibia."

**BAADA HOSPITALI**

Kifamilia, anajitambulisha alikuwa na mke na watoto wawili, ambao sasa ni wanachuo cha elimu ya juu nchini na mkewe, waliopata ajali wote, Shamba analalamika kukimbiwa na mwenza huyo, katika maisha baada ya ajali.

"Mimi nina familia, inanibidi niwahudumie watoto wangu licha nipo katika hali hii. Gari inavyopata ajali nilikata bima ndogo hawakuweza kunilipa,"anasema.

Mtaalamu wa Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), Dk. Lutfi Abdallah, anasema mtu anavyopata ajali mbaya, muokoaji asipomnyanyua vizuri, kuna uwezekano wa madhara zaidi, hata kifo.

"Kuna nchi nyingine mtu amepata ajali wanavyokuja askari ama zimamoto au waokoaji, wanaelewa jinsi ya kukubeba, ili asimsababishie madhara mgojwa aliyepata

Endelea Uk. 12

AFYA

Na Yasmine Protace, aliyekuwa Dodoma

# Umma wafunguka macho ukatili jinsia unavyowamaliza afya zao

## •Nini kinafuata? Waonyeshwa pa kupita

MATUKIO ya ukatili wa kijinsia, yamekuwa yakiripotiwa kila mara nchini na nje ya mipaka, huku kukiwapo sura upande wa pili, vita vinakabiliwa kwa njia ya utoaji elimu na mikakati mtambuka kitaifa, hata kimataifa.

Wapo wanaofanyiwa ukatili huo, lakini hawana pa kusemea, japo serikali kumewekwa mazingira rafiki ya kutoa taarifa hizo ili wahusika wachukuliwe hatua.

Moja ya maeneo yanayopokea malalamiko hayo ni katika madawati ya kijinsia, ili wahusika wa makosa wachukuliwe hatua za kisheria.

Katika kuchangia juhudi hizo, asasi ya Restress Devolopment, imebuni mradi na kuupeleka jijini Dodoma, ili jamii ipatiwe elimu ya kuwakomboa na vizazi vyao, ukipewa jina la 'Tutimize Ahadi.'

Hapo kuna vijiji vya wilaya za Bahi mkoani Dodoma, vilinufaika, kwa jamii kupatiwa elimu ya uzazi salama, ipambane dhidi ya matukio ya ukatili.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Lamaiti,Yunus Magembe, anasema kabla mradi kuchukua nafasi, ukatili wa kijinsia ulishamiri, akitaja matukio ya wajane kurithiwa, kutoshiriki uamuzi, vipigo kwa wake na vijana kiume kuamini masuala ya uzazi hayawahusu.

Magembe, katika taarifa yake kwa wanahabari, anafafanua mradi wa 'Tutimize Ahadi':

"Kabla ya mradi kuwapo, matukio yalikuwapo katika kata hii ya Lamaiti, ambapo jamii ilikuwa haijui haki zao na kujikuta wakifanyiwa ukatili."

Anaongeza, awali kulikuwapo ukatili wa kipigo, pia wajane kurithiwa hasa waume zao waliposhirikishwa katika uamuzi mkubwa, mila na desturi tata ziliwakandamiza wajane.

Pia, anataja akiitacho 'ukatili wa kiuchumi' uliokuwapo kipindi cha nyuma, mume na mke wanazalisha mali, lakini inaangukia mshangao, mmoja anauza mali bila ya kumshirikisha mkewe.

Magembe anasema, baada ya kuanzishwa kwa mradi na kutolewa elimu, hivi sasa wajane wameanza kujitambua kuzijua haki zao, pia vijana wa kike na kiume wanashiriki katika vituo vya afya na kupatiwa elimu ya masuala ya uzazi salama.



Zuwena Bakari, askari polisi wa Kitengo cha Jinsia Kituo cha Kati Dodoma, akifafanua jambo. **PICHA: YASMINE PROTACE.**

Anataja eneo lingine, ni mradi unaosaidia kupunguza matukio ya kikatili, kwani kuna kamati zenye wajumbe zilizoanzishwa na wateuliwa wenyeviti wa kama za kusuluhisha migogoro.

Hapo inajumuisha wajumbe kutoka polisi kata, watu mashuhuri kutoka jinsia zote na viongozi wa dini wasiopungua 18.

**POLISI JAMII**

Askari Polisi anayetajwa kwa jina la Domama, kutoka Dawati la Jinsia, anasema kwa sasa wanaendelea kupambana nayo, akifafanua kuwa wanafunzi wa kidato cha pili na tatu, wamekuwa wakiripotiwa ni miongozi mwa wanafunzi wanaopata mimba za utotoni.

"Wanafunzi hao ni wale wenye umri kati ya miaka 15 na 16. Kesi zinazokuja kwetu, ambazo zinaongoza kwa kuripotiwa, ni kesi za mimba ndio zimeshika nafasi huku zikifuatiwa na kesi za ukatili wa kijinsia," anasema.

Anaongeza kuwa katika kesi hizo za mimba, wengi wao ni wanafunzi wenye miaka 15 hadi 16 na wanasoma kidato cha pili na cha tatu, akifafanua zaidi:

" Jamii awali ilikuwa haitoi taarifa inapofanyiwa matukio ya kikatili na hata kutoa taarifa watoto wanapokatiza masomo, kwa kupata ujauzito, lakini baada ya kuanzishwa mradi wa 'Timiza hadi'ulioletwa na Restless, jamii wamepata mafunzo na wameweza kujitambua."

Huku akidokeza wanaume nao wamo salama katika jiji la likizo ya ugonjwa wa corona, nayo haikuwaacha salama wanafunzi, baadhi yao waliopata mimba.

Pia, askari huyo anaeleza kuwapo changamoto ya kukosekana ushahidi unaohusu ukatili, mimba za ututoni na ubakaji na hari hiyo, inachangia kuharishwa kwa kesi ikiwamo na kuchelewa kuisha kwa kesi.

**UFUATILIAJI**

Nipashe imeshuhudia ziara ya ukaguzi wa kiserikali, ambako serikali ya kijiji cha Mundemu, wilayani Bahi Mkoa wa Dodoma, imeweka utaratibu wa kila mjamzito asipohudhuria kliniki, anaadhibiwa jukumu la kufanya usafi mahali hapo na mumewe.

Hiyo ni baada ya kubainika kuna wajawazito wanashindwa kuhudhuria kliniki pasipo sababu, hali inayochangia matatizo mama anapojifungua.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mundemu, Stephen Daudi , anasema:"Kijijini umeleta mabadiliko makubwa kwa jamii, awali matukio ya ukatili, afya ya uzazi wananchi wa hiki kijiji walikuwa hawajitambui hivyo elimu ilipoanza kutolewa kupitia mradi huo jamii iliweza kujitambua."

Kiongozi huyo anasema, wanaofanyiwa ukatili, wameshaanza kutoa taarifa na wahusika wanachukuliwa hatua, jamii inajitambua katika afya ya uzazi jamii inajitambua, vijana wanafika vituo vya afya na kupatiwa elimu ya uzazi wa mpango.

Anasema elimu ya uzazi, serikali ya kijiji imekuwa ikiwahamasisha wajawazito kushiriki vituo vya afya na wenza wao, ili wahudhurie kliniki kila wanapotakiwa kwenda.

Mwenyekiti huyo, Daudi anasema hatua yao ni kumfuatilia mama mjamzito na mwenza wake kama wanaenda kliniki na wakibaini hawaenda wanawakamata na kuwapeleka kufanya usafi katika kituo cha afya.

"Wapo baadhi ya wajawazito na wenzao wao, ambao wanakaidi kuhudhuria kliniki, nasi tukibaini hilo, tunawafuatilia na kuwakamata na kuwapa eneo katika kituo cha afya ili wafanye usafi siku nzima," anasema.

Pia, anataja adhabu ya usafi ni hatua iliyozaa matunda makubwa katika kuimarisha mahudhurio ya kliniki kwa juu, manufaa zaidi yakishuhudiwa kwa mama kujifungua salama.

**WADAU**

Amina Mahiya, wakili mtetezi uwajibikaji kutoka Kata ya Kikuyu Kaskazini anaeleza kuwapo mafanikio katika awamu ya pili iliyoanza mwaka jana na unakamilika mwezi huu, huku uliotangulia wa kwanza, ulianza katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Wakili Amina, anasema wamebaini kuwapo mtazamo mwingine ulioko katika itikadi za vijana, wakiamini kwamba masuala ya uzazi yanaishia mikononi mwa watoto pekee, ilhali ukweli ni kwamba yanaangukia sura tatu, wazazi baba na mama, pia binti.

Anasema, ni hatua iliyochangia kuongezeka bajeti inayotakiwa katika sekta hiyo ya afya, baada ya kufanikiwa kushawishi vikao vya kiserikali kuridhia maboresho hayo fedha kuhusu uzazi kuingezwa.

Pia, Amina anasema katika mtazamo maalum dhidi ya ukatili wa kijinsia, jamii imejitambua na kutoa ushirikiano kufanikisha wakiukaji kukamatwa.

Katika hilo anaelekeza shukrani kwa watendaji wa serikali kuanzia ngazi za kata hadi juu, kwa namna walivyo msaada mkubwa katika kufanikisha mradi kutimia katika namna sawia.

# MAJERUHI AJALI GARI KUPINDUKA MARA 3 ALIVYOPEWA MAISHA MAPYA

Inatoka Uk. 11

ajali," anasema Abdallah.

**MWANASHERIA POLISI**

Mwanasheria wa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Mrakibu Deus Sokoni, anasema elimu inayotolewa ya usalama barabarani kwa kushirikiaa na wadau wengine, imesadia kupunguza ajali nchini.

Anasema mapambano ya ajali za barabarani kwa miaka iliyopita kuanzia 2009 zilikuwa nyingi na kuna mwaka zilifika 27,000, vikiwa na vifo 16,000.

Mrakibu Sokoni anataja mwaka 2018 walipunguza ajali kwa asilimia 28, akiwa na takwimu jumla za ajali 3,732 yenye vifo 1,788.

Pia, mwaka jana, ilikuwa na ajali 2704 na vifo 1449, ambayo ni punguzo la vifo 348.

"Mwaka 2018 kulikuwa na majeruhi 3,746 kabla ya hapo tulishawahi kufikia zaidi ya majeruhi 20,000 walikuwa wengi ajali zinavyopungua na majeruhi wanazidi kupungua. Mwaka 2019 tukawa na majeruhi 2834," anasema Sokoni.

Sokoni anadokeza mwaka huu hadi mwezi Juni, kulikuwapo ajali 978, yenye vifo 616, wakati mwaka jana kipindi kama hicho kulikuwapo vifoli 744. Maana yake ni kupungua vifo 128

**MZIZI WA AJALI**

Sokoni anataja makundi yaliyoathirika zaidi katika kipindi ni madereva 73 na mwaka uliotangulia 79.

Aidha, anasema vyanzo vya ajali vinavyosababishwa na binadamu ni asilimia 76 na kwa madereva asilimia 99. Madereva waliojeruhiwa mwaka 2019 walikuwa 149 na mwaka huu wako 103

Sokoni anaeleza abiria waliokufa kwa kisa hicho mwaka jana ni 247 na mwaka huu 229, hapo kukiwapo upungufu wa 18 mwaka huu.

"Abiria waliojeruhiwa Januari hadi Juni mwaka 2019 walikuwa 843 na Januari hadi Juni 2020 waliojeruhiliwa ni 685 tumepunguza majeruhi 158," anasema Sokoni.

Anawataja madereva wa bodaboda waliokufa ni 157 kuanzia Januari hadi Juni mwaka jana na mwaka huu, 124, upungufu ni vifo 33, huku majeruhi waendesha pikipiki wa nusu mwaka uliopita ni 252 na mwaka huu 167

**MATATIZO NA ADHABU**

Sokoni anasema mwaka huu, Polisi imeshafungia leseni 37 za madereva wa mabasi nchini, kwa makosa mbalimbali.

"Kuwafungia kumesaidia kuogopa kusababisha ajali tumejipa mamlaka ili tuweze kuwadhibiti kama akiendesha ovyo barabarani tukiwa na ushahidi ninamuita, namhoji akikubali namuambia aende kusaidia kulea watoto nyumbani kwa miezi mitatu," anasema

"Kuna dereva wa kike aliendesha basi kwa fujo barabarani ili akamatwe aletwe kwangu kwa makusudi tu.

"Anaeleza nilifanya kusudi ili nikamatwe niletwe kwako nieleze malalamiko yake kwa kuwa ameyapeleka sehemu husika hayafanyiwi kazi," anasimulia.

Sokoni analalamika kuna shida ya watu kuchelewa, baadhi ya abiria walipata ajali kwa zaidi ya 15, ndio wanajitokeza kudai fidia, ikiwa ni ishara ya bado kuna upungufu.

**KUPUNGUZA AJALI**

Mratibu wa Masuala ya Usalama Barabarani kutoka Shirika la Afya Dunia (WHO), Mary Kesi, anasema wamekubaliana kwa muongo wa pili, wamekusudia kupunguza nusu ya ajali zilizopo.

Hata hivyo, anakiri hawajafanikiwa kumaliza lengo kama hilo cha asilimia 50 kipindi cha miaka 10 kilichopita.

Analalamika kuwapo tatizo la upatikanaji taarifa za ajali na asilimia 10 ya vifo vinatokea katika vituo vya afya, hivyo kuna uwezekano wa kukosa taarifa kwa usahihi, hivyo yote yanaingia katika tafakuri ya watakachokifanya.

AFYA

USHUHUDA WA MBEYA...

# Ilivyo janga la kiafya kwa watoto kuendekeza maeneo ya starehe

- Chanzo kikuu wazazi wanaojisahau
- Polisi walia ukiukaji 'utii bila shuruti'

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

“KILA siku ya Jumapili baada ya kutoka kwenye ibada, lazima nitoke na wanangu 'out' (matembezini), kwa maana ya kwenda kula na kunywa pamoja na familia yangu. Siku hiyo wanangu nawapeleka sehemu nzuri ambayo ina muziki mzuri na mandhari ya kuvutia.

“Hakuna muda maalum wa kurudi nyumbani, bali itategemeana na mazingira tutakayoyakuta huko matembezini au baa, muhimu ninachozingatia kama mama ni kuhakikisha wanangu hawatumii kilevi chochote, isipokuwa watakula na kunywa kadri watakavyotaka.

“Unavyokuwa maeneo ya starehe unanogewa. Huoni hata kama muda umeenda kuja kushtuka unashangaa inafika saa tatu ya usiku, hapo watoto hawajaandaliwa nguo za shule, wala kufanya kazi walizoachiwa na walimu wao pamoja na maandalizi mengine ya shule,” anaeleza Juliana (jina la pili tunalo), mama wa watoto watatu jijini hapa.

Anaendelea:“Sitasahau siku tumetoka na wanangu tulinogewa pale hotelini, maana kulikuwa na tamasha ikafika hadi saa tano, muda huo watu wamelewa kuna vurugu, baadhi ya matendo yaliyokuwa yanaendelea ni ya aibu hadi wanangu wakawa wanahoji.

Mwingine, Japhet Mwazembe, mfanyabiashara jijini Mbeya, ana maelezo kwamba kila mwisho wa wiki, au kawaida ya kutoka na watoto wake kwenda matembezini, husani maeneo yenye michezo ya watoto na huko anahakikisha wanafurahia kutosheka na burudani wanazozipata.

Anasema, licha ya kufanya hivyo kwa ajili ya kuwapatia furaha watoto wake, anakiri kutozingatia muda kwa watoto na wanaachwa hadi watosheke, pasipo kupewa mipaka ya muda.



Watoto wakifurahia jambo mjini Mbeya. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

### WASIMAMIZI SHERIA

Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Kyela, Paul Mabula, anasema Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, inapinga mtoto kuhudhuria yenye shughuli zinazovunja utu wake, sambamba na wasihudhurie matamasha au shughuli hizo nyakati za usiku.

Anahimiza, sheria inampa nafasi mtoto kushiriki shughuli zinazolinda hadhi yake mchana pekee muda usiozidi saa 12 jioni na ombi lake ni jamii izingatie matakwa ya Sheria ya Usalama na Utu wa Watoto wawapo katikamaeneo ya starehe, badala ya kukaa nao usiku maeneo hayo ya starehe.

“Kifungu cha 158 cha mwaka 2009, kinatoa zuio kwa mtoto kushiriki kwenye maonyesho au sherehe zozote, kwa sababu ni kosa kisheria bali wakati wa mchana anaruhusiwa,” anasema Mabula.

> Anaongeza kuwa Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, inaeleza kuwa mahali popote mtoto anakohudhuria kusiwe na mambo au kuonyeshwa vitu vinavyovunja utu au haki zake, kulingana na hao waliopo.

Anaongeza kuwa Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, inaeleza kuwa mahali popote mtoto anakohudhuria kusiwe na mambo au kuonyeshwa vitu vinavyovunja utu au haki zake, kulingana na hao waliopo.

Baadhi ya wananchi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, akiwamo Justine Mwakyusa, anashauri sio vyema mtoto kushiriki maeneo ya starehe iwe mchana au usiku, kwa sababu kuna watu wanafanya mambo yasiyo na mwelekeo sahihi, ilhali kuna watoto katika maeneo hayo.

Licha ya kushiriki katika maeneo ya starehe lakini pia watoto wachanga waopelekewa maeneo hayo wanaweza kupata madhara kiafya, kunapokuwapo muziki wenye sauti kubwa, hupenya kwenye masikio ya watoto.

Kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Namba 21 ya Mwaka 2009, inataja wajibu wa wazazi, walezi na jamii kuhakikisha watoto wanapata haki zao za msingi, ikiwamo elimu.

Sheria hiyo inasisitiza jamii inabeba wajibu wa kufuatilia na kuhakikisha watoto wanaandikishwa na kwenda shule, pamoja na kufuatilia maendeleo yao masomoni, huku ikiwa na kipengele kinachoeleza kuhakikisha mahudhurio na kusoma kwa bidii.

Licha ya Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 kuweka wazi kwamba ni kosa mwenye umri chini ya miaka 18 kuwa katika maeneo ya starehe nyakati za usiku, bado kunashuhudiwa baadhi ya wazazi kukiuka sheria hiyo, ama kwa kujua au kutokujua.

Ni aina ya agizo la kisheria linaloendana na marufuku ya ajira kwa watoto katika maeneo hayo yanayotajwa, mfano katika baa, kunawezeakana mabaya kushuhudiwa matusi, mavazi yasiyoendana na heshima, hata yakamjengea picha na saikolojia mbaya mtoto.

### WAONAVYO WANANCHI

Wananchi wa Mbeya waliozungumza na Nipashe kuhusu suala hilo, walikuwa na maoni kwamba mwenendo wa kuwapeleka watoto kwenye maeneo ya starehe, kunaweza kuhatarisha usalama wao, mathalan endapo kunatokea vurugu na watu kurushiana chupa au vingine vya hatari.

Kwa mujibu wa Jeshi la Polisi- Dawati la Jinsia mkoani Mbeya, mara nyingi wamekuwa wakifanya doria kwenye maeneo mbalimbali ya starehe, lengo mojawapo ni kukagua usalama wa watoto katika maeneo hayo usiku.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, anasema baadhi ya wazazi na walezi wamekuwa wakikaidi zuio hilo la kisheria kwenye maeneo ya starehe usiku na wanapowakuta huwaondoa watoto mara moja, kwani kuwaacha ni kuwaingiza katika tabia mbaya.

### MWISHO WA MWAKA?

Wakati ikielekea msimu wa sikukuu na kumaliza mwaka msimu ambao wa huambatana na furaha zisizo na kifani, furaha ambazo huiweka sawa miili na akili za watoto hususani, mara baada ya kutoka masomoni.

Vilevile, furaha zinazojumuisha utolewaji na upokeaji zawadi miongoni mwa wazazi na watoto, ama ndani au nje ya familia. Ushauri uliopo, ni kwamba furaha za sikukuu na zinginezo kwa watoto hazipaswi kupitiliza hata kuharibu njia sahihi za malezi ya watoto, licha ya tabasamu ya mzazi ni kuona mtoto anafurahi

Uzoefu unaonyesha watoto wanatendewa matukio ya kikatili mara nyingi zaidi katika vipindi na mazingira ya sherehe na sikukuu na hasa zinapoendena na likizo za masomo.

Aidha, kuna ufafanuzi wa kijamii kwamba, wazazi wengi wanaomiliki simu za kisasa maarufu 'simu janja' watatamani kuwasiliana kijamii kupitia simu hizo, wakiwa na watoto maeneo ya starehe



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei.

MAZINGIRA

# Wazalishaji Coca-Cola rasmi kusafisha fukwe unaochafuliwa na utitiri plastiki

**Na Elizabeth Zaya**

'MCHANGA Pekee' ni kampeni inayolenga kukuza ukusanyaji chupa za plastiki na uhifadhi wa bahari, kampeni iliyoanzishwa baada ya kubaini asilimia kubwa ya taka baharini zinatoka pwani kupitia mtoni, mifereji ya maji na fukwe. huku ikikadiriwa kila kilomita ya mraba ya bahari ina vipande 13,000 ya vifaa vya taka za plastiki.

Utafiti wa hivi karibuni uliofanywa na Baraza la Kimataifa la Vinywaji (ICBA), uligundua kuwapo vipande milioni 15 vya taka za plastiki baharini kwa sasa.

Ripoti kutoka asasi ya Ocean Conservancy's 2018 International Costal Cleanup, inasema wakati usafishaji pwani, vichungi vya sigara viko kwa wastani wa vipande milioni 2.4, inafuatiwa na vifuniko vya chakula kwa wastani wa vipande milioni 1.7.

Pia, kunatajwa kuwapo chupa za plastiki milioni 1.6, vifuniko vya plastiki milioni 1.1 na mifuko ya plastiki vipande 757,523 vinavyounda vikundi vitano vya uchafu uliokusanywa wakati wa kusafisha pwani uliofanywa na nchi zaidi ya 100 ulimwenguni.

Nchini kunatajwa pwani za Mtwara, Dar es Salaam, Bagamoyo, Tanga na Zanzibar zina sura na hali zinazofanana, kwa kuzingatia shughuli za kibinadamu na chupa zisizofaa za plastiki zinazotupwa kwenye njia za maji za mito na mifereji, vyanzo vikuu cha uchafuzi.

Ni aina ya mtazamo kwamba hiyo haitoshughulikiwa na inakadiriwa ifikapo mwaka 2050, huenda bahari itakuwa na vifaa vya plastiki nyingi zaidi, hali ambayo si rafiki kwa ustawi wa samaki.

**COCA-COLA YAAMUA**

Kutokana na hai hiyo, kampuni inayozalisha vinywaji baridi ya Coca-Cola Kwanza, iliamua kuchukua hatua ya kuanzisha kampeni maalum ya kupambana na uharibifu wa mazingira inayojulikana kama 'Mchanga Pekee'.

Ni kampeni iliyoanzishwa mwaka jana, ikilenga kufundisha, kushirikisha na kushawishi jamii namna bora ya utupaji taka za plastiki kupitia kusafisha pwani, ukusanyaji chupa za plastiki, kuchakata na kutupa chupa za plastiki nchini.

Tangu kuanzishwa kwa kampeni hiyo, Coca-Cola Kwanza imekuwa ikielimisha jamii namna ya kufanya usafi na kupeana maarifa inayowaweka katika mazingira salama, kwa ajili ya kukomboa mchanga wa Pwani kutokana na taka za plastiki zisizo za lazima, hivyo kuokoa ikolojia ya mazingira.

Mkurugenzi wa Masuala ya Umma na Mawasiliano wa Coca-Cola Kwanza, Haji Mzee, anasema kampeni ya 'Mchanga Pekee' imegawanywa katika shughuli kuu mbili, zote zinaonyesha lengo la pamoja kuelimisha jamii kupitia kujihusisha na uhifadhi wa mazingira na kikuu katika kampeni ni kusafisha pwani na kununua chupa za plastiki kwa ajili ya kuzichakata.

Pia, anasema kampeni imejengwa katika kuhamasisha jamii kufuatilia usafishaji pwani kote nchini kwa kufuata utaratibu wa kuzuia uchafuzi



Kampeni ya kusafisha ufukwe ikiendelea, katika picha tofauti. **PICHA: MTANDAO.**



Mkurugenzi wa Mawasiliano Coca-Cola Kwanza, Haji Ally Mzee, alipozungumza jijini Dar es Salaam, wakati wa uzinduzi wa kampeini ya Mchanga Pekee. **PICHA: ELIZABETH ZAYA.**

unaosababishwa na utupaji holela wa chupa za plastiki na namna ya kutunza mazingira.

**AJIRA MPYA**

Anasema ni kampeni iliyofanikiwa kuajiri kundi kubwa la watu, wakiwamo wanawake wanaofanya kazi hiyo ya usafi, mara tano kwa wiki.

"Wanawake wanaofanya kazi hiyo wamepatiwa mikataba kabisa, kwa mfano katika fukwe ya 'Coco Beach' (Oysterbay Dar es Salaam) huwa wanasafisha kila Jumamosi, Jumapili, Jumatatu, Jumatano na Ijumaa," anasema Haji.

"Kupitia kazi hii, timu ya wasafishaji wa pwani, imebaini kuwapo idadi kubwa ya vipande vya chupa za plastiki katika maeneo hayo, nyingine zikiwa pini, sindano, vifuniko vya chakula, majani, vifungio vya plastiki, mifuko ya kubeba plastiki pamoja na makombo ya chakula," anfafanua

**M AVUNO YAKE**

Haji anasema, kampeni hiyo imefanikiwa kufikia watu wengi katika jamii na kwamba kila mwisho wa wiki, ufukwe wa Coco Beach pekee hupokea kati ya watu 300 hadi 500.

"Kupitia kikundi chetu cha kusafisha pwani, makadirio ya chupa za plastiki 150, zaidi ya vifungashio 250 vya plastiki na idadi kubwa ya uchafu wa baharini uliohamia pwani na mawimbi yenye nguvu ya bahari, zilikusanywa," anaeleza Haji.

Anasema mpaka sasa, wafanyakazi wa kampeni hiyo wamefanikiwa kukusanya taka za chupa za plastiki zaidi ya 8,500 karibu na Coco Beach na zote zimepelekwa katika kampuni za kuchakata kutengeneza bidhaa za plastiki.

Haji anasema, pia kampuni ya Coca-Cola Kwanza iliamua kuanza kununua chupa za plastiki kwa bei Sh. 50 kila moja, lengo ni kuipa jamii fursa kwa jamii kutambua umuhimu wa kutunza mazingira na kutumia taka kama fursa ya kujipatia kipato.

Anasema, mpaka sasa kampeni hiyo imeshafanikiwa katika maeneo mbalimbali jijini Dar es Salaamm ikiwa ni pamoja na Mbagala wilayani Temeke, Manzese wilayani Ubungo na Tandale wilaya ya Kinondoni.

Maeneo mengine anayataja kuwa Mwanyamala, Kinondoni, Buguruni na kila eneo kampeni imesaidia kutoa elimu ya mazingira ikifikia wakazi takriban 5,000 na hadi sasa, zaidi ya chupa za plastiki 60,000 zilizotumika zimeshanunuliwa na waendesha kampeni hao.

"Bei inayotumika kwa ununuzi wa chupa katika kampeni hii ni mara nne ya bei ya soko. Wafanyabiashara wengine hununua chupa za plastiki zilizotumiwa kwa msingi wa uzito wao ambapo kilo moja ya chupa ya plastiki huuzwa kati ya Sh.200 na Sh.250.

"Kilo ya chupa za plastiki zilizotumiwa zina vipande kati ya 25 na 30, ambazo, ikiuzwa kwa kipande kupitia kampeni yetu, mtu angepata kati ya Sh. 1,000 na Sh.1, 500,"

"Kampeni hii imewawezesha wananchi wengi kiuchumi kwa sababu imekuwa ikipokelewa vyema na jamii. Watu wengi huja na chupa za plastiki zilizotumiwa," anasema Haji, lengo la kampeni ni kuijengea jamii hamasa na kupeana elimu ya namna boraya uhifadhi na usimamizi endelevu wa mazingira.

Pia, anaeleza anaunga mkono serikali katika kuunda jamii bora ambayo inachukua umuhimu wa uhifadhi wa mazingira na usimamizi endelevu wa mazingira hayo kutoka moyoni.

"Tunaamini kwamba kujenga tabia ya utunzaji endelevu wa mazingira utaongeza idadi ya watalii hususani katika fukwe zetu," anasema Haji na kuongeza:

"Kwa sababu hakuna mtu anayependa kwenda kutembelea mahali pachafu, lakini mazingira yetu yakiwa safi muda wote tutapata wageni wengi zaidi."

Pia, tutakuwa tunaendelea kutengeneza mazingira kwa wanawake na vijana wetu kupata fursa ya kujipatia kipato na ajira.

"Tunaamini kwamba, tutakuwa tumepunguza kwa kiwango kikubwa taka za chupa za plastiki katika jamii na kuelimisha kwa sababu jamii itakuwa imepata elimu ya kutosheleza.

"Ulinzi na uhifadhi wa ikolojia ya baharini na ardhi inayolimwa nayo itakuwa imetunzwa, hivyo kuwezesha jamii yetu kuishi katika mazingira ambayo hayana uchafuzi wa mazingira," anasema.



# Wabunge wanolewa diplomasia na itifaki

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WABUNGE wamepewa somo la diplomasia na itifaki ili kutekeleza vyema majukumu yao ya kibunge.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, alitoa somo hilo jana kwa wabunge hao wa Bunge la 12 lililozinduliwa hivi karibuni na Rais John Magufuli.

Alisema kuna umuhimu mkubwa kwa wabunge kutambua masuala yote ya kidiplomasia na kuiitifaki ikiwamo mavazi na upeperushaji bendera.

"Kwa ujumla kuhusu dhana ya itifaki, ya viongozi wa kitaifa, katika mawasiliano ya viongozi, Itifaki ya mawasiliano rasmi na balozi zilizopo nchini, pia kuna itifaki ya upeperushaji bendera na mipaka yake, ya mavazi kwa viongozi pamoja na mambo mengine kuhusu wabunge na viongozi wote nchini," alisema.

Alibainisha kuwa somo hilo linalenga kuwajengea wabunge uelewa mpana zaidi kuhusu masuala ya diplomasia na itifaki ikiwa ni moja ya masuala muhimu ya kuyafahamu kama zilivyo sheria na taratibu.

Alisema masuala hayo watakutana nayo katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya kibunge.

# Mavunde aanza kutekeleza ahadi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MBUNGE wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, ameanza kutekeleza ahadi alizotoa kwenye uchaguzi mkuu 2020 ya kutatua tatizo la maji.

Anesema amechimba visima sita kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo Chigongwe.

Akikagua jana uchimbaji wa kisima cha maji katika Kata ya Chigongwe, Mavunde, alisema hicho ni kisima cha sita kuchimbwa tangu achaguliwe kuwa mbunge wa jimbo hilo, kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

"Naendelea kutekeleza ahadi nilizotoa kwa wananchi juu ya utatuzi wa kero ya upatikanaji wa majisafi na salama," alisema.

Diwani wa Kata hiyo, Simon Machela, alimshukuru Mavunde kwa kutekeleza ahadi yake na aliahidi kabla hajaanza shughuli zingine ataanza na utatuzi wa tatizo la maji.

Alisema Mtaa wa Ng'ambala hawapati kabisa maji, hivyo kupitia mradi huo watapata maji na kuondokana na kilio chao cha kila siku.

Baadhi ya wakazi wa Chigongwe walieleza kufurahishwa na jitihada hizo, na kwamba kero ya maji ilikuwa kubwa.

Neema Joseph, alisema kata hiyo ina mitaa mitatu ambayo yote ilikuwa inakabiliwa na tatizo la maji, hivyo hatua hiyo imesaidia kupunguza adha hiyo.

# Ujangili hifadhini wapungua kwa 70%

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa ujangili katika hifadhi za taifa na maeneo tengefu nchini umepungua kwa asilimia 70 katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Allan Kijazi, aliyasema hayo alipokuwa akifungua mafunzo kwa watendaji wa wizara hiyo jijini hapa, yaliyoandaliwa na serikali kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la PAMS Foundation linalojihusisha na mapambano dhidi ya ujangili.

Dk. Kijazi alisema kupungua kwa ujangili ambao ulikithiri mwaka 2007 hadi 2015 kumechangiwa na operesheni mbalimbali zilizofanyika kwenye maeneo hayo.

Alisema kwa kipindi hicho watu zaidi ya 30,000 wamekamatwa kwa tuhuma za kujihusisha na ujangili.

"Kwa miaka mitano iliyopita, operesheni zilizofanywa na serikali na vikosi vya kuzuia ujangili pamoja na wadau wote, zimefanikisha kukamatwa kwa majangili 33,386 na silaha mbalimbali 2,501 zikiwamo silaha za kivita," alisema.

Hata hivyo, alionya watumishi watakaobainika kutokuwa waaminifu hatua kali zitachukuliwa dhidi yao.

Kadhalika, alisema serikali imejipanga kuandaa na kutekeleza mpango mkakati wa kitaifa wa kudhibiti ujangili, lakini kuundwa kwa Jeshi la Uhifadhi Wanyamapori na Misitu.



Mchuuzi wa vikapu akitembeza bidhaa zake katika eneo la stendi ya daladala ya Sabasaba, jijini Dodoma jana. Kikapu kimoja alikiuza 3,000/-. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Ombi Jiji kupanua stendi ya Sabasaba

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imeombwa kupanua eneo la kituo cha daladala cha Sabasaba ili kupunguza msongamano wa magari nje ya kituo hicho.

Mkazi wa Jiji hilo, Diana Lameck, akizungumza na Nipashe kwenye kituo hicho, alisema kumekuwapo na kero na kusababisha magari madogo kushindwa kutumia barabara ya Sabasaba kutokana na msongamano wa daladala kwenye barabara hiyo.

Alisema mbali na kero hiyo, pia watumiaji wengine wanakumbana na adha hiyo hasa wanaopita kuingia Kituo cha Afya Makole, Shule ya Sekondari Dodoma na maeneo mengine jirani.

"Yaani hata abiria wa daladala wanalazimika kushukia nje ya stendi kutokana na foleni ndefu ya magari na hii hali ni wakati wa asubuhi na jioni, yaani kituo ni kidogo kwa wingi wa magari uliopo," alisema.

Aliomba uongozi wa jiji hilo kuangalia eneo ambalo litafaa kuwa kituo cha daladala ili kuiondoa msongamano kwenye eneo hilo ambalo pia linatumika kama soko.

Naye Halima Ali, alisema ndani ya kituo hicho eneo la kuegesha magari limekuwa dogo kutokana na wafanyabiashara wadogo kusogea kwa kiasi kikubwa na hivyo magari kukosa eneo la kuegesha.

"Wafanyabiashara wadogo wanasogea eneo la kuegesha daladala hali ambayo inahatarisha hata usalama wao, inabidi Jiji waliangalie hili," alisema.

Akizungumzia adha hiyo, Katibu wa Soko la Sabasaba, Abuu Mohamedi, alisema tatizo hilo linachangiwa na wafanyabiashara kutoheshimu mipaka ya eneo la soko.

Alisema wametoa elimu kwa wafanyabiashara hao, lakini wamekuwa wakikaidi, jambo ambalo ni hatari kwao na bidhaa zao.

"Wafanyabiashara wote wamehama eneo lao husika la kufanyia biashara na kuvamia eneo la stendi ya daladala, hili eneo ni kubwa isipokuwa ni tatizo hilo tu linafanya daladala kukosa eneo la kuegesha kwa ndani na kuegesha nje kwenye barabara," alisema.

Aliongeza: "Gari linaweza kufeli breki huku umepanga bidhaa zako chini ni hatari hata kwa afya zetu na ikizingatiwa kwa sasa kuna mvua, magonjwa ya mlipuko yanaweza kutukuta na kuathiri, ukiwaambia wanasema hali mbaya lazima wafanye biashara kwenye msongamano wa watu."





# Ujazo maji Ziwa Rukwa waongezeka

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

UJAZO wa maji katika Ziwa Rukwa umeongezeka kutoka wastani wa mita za ujazo 5.8 mwaka jana mpaka mita 7.5 kutokana na mvua kubwa iliyonyesha msimu wa 2019/20 katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Aidha, ongezeko hilo la maji linadaiwa kuchangiwa pia na ongezeko la utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji vya mito inayomwaga maji kwenye ziwa hilo katika miaka ya karibuni.

Mtaalamu wa Maji kutoka Bonde la Ziwa Rukwa, Nasra Nasoro, aliyasema hayo juzi kwenye kikao cha wadau wa maji ya bonde hilo kilichofanyika katika Wilaya ya Chunya kwa lengo la kujadili matatizo mbalimbali yanayolikabili bonde hilo.

Alisema kiwango hicho cha ongezeko la maji kwenye ziwa hilo, hakijawahi kutokea katika kipindi cha miaka 20 iliyopita kutokana na matatizo mbalimbali yaliyokuwa yanaviandama vyanzo vya maji.

"Haya ni mafanikio makubwa sana kwetu pamoja na wadau wetu wote. Ongezeko hili la mita za ujazo 1.3 ni kiwango kikubwa sana na ni changamoto kwetu kuendelea kuimarisha uhifadhi wa vyanzo ili maji yasipungue tena na sasa hivi ni mwezi Novemba bado maji yako juu," alisema Nasoro.

Alisema katika miaka ya hivi karibuni, kiwango cha maji kwenye ziwa hilo kilikuwa kimepungua kiasi cha kuanza kuleta wasiwasi wa ziwa hilo kutoweka miaka ya baadaye, lakini ongezeko hilo limeleta matumaini mapya.

Nasoro aliwapongeza wadau mbalimbali wa mazingira ambao wamekuwa wakishiriki kutunza mazingira ambayo ndiyo chanzo cha maji yanayotiririka kuingia kwenye ziwa hilo.

Naye Ofisa Mazingira wa Wilaya ya Chunya, Yohana Mguluka, alisema wilaya hiyo ni miongoni mwa maeneo yenye vyanzo vingi vya maji ya ziwa hilo na kwamba mwaka huu kuna mito mingi ambayo imetiririsha maji mwaka mzima.

Alisema kutokana na ongezeko hilo, kuna hatari ya kutokea mafuriko kwa wakazi wanaoishi jirani na ziwa hilo kwa madai kuwa maji bado yanazidi kutiririka kwenda kwenye ziwa na mvua tayari imeanza tena kunyesha.

Aliiomba Bodi ya Maji ya Ziwa hilo kuanza kuweka tahadhari za kutokea mafuriko ikiwa ni pamoja na kuhamasisha wananchi kuyatumia maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

"Kiwango cha maji kinasoma juu, lakini ukiangalia mwezi huu tayari mvua imeanza kunyesha tena na wataalamu wametabiri kwamba kutakuwa na mvua nyingi tena mwaka huu. Tujiandae kukabiliana na mafuriko ambayo yanaweza yakaleta madhara kwa watu," alisema Mguluka.

Nao baadhi ya wadau walidai kuwa moja kati ya matatizo ya maji ya ziwa hilo, yanayosababishwa na shughuli za kibinadamu hasa kwa vyanzo vilivyoko wilayani Chunya ni uchafuzi wa maji kutokana na shughuli za uchimbaji wa madini.

Mmoja wa wadau hao, Lucy Omary, alisema kipindi cha mvua baadhi ya wachimbaji wadogo huwa wanafanya shughuli za kuchimba madini kwenye mito na hivyo kusababisha maji hayo kuchafuliwa.



Mwanachama wa Young Feminist Forum, ambao ni wanaharakati wa kutetea vijana dhidi ya masuala ya kijinsia chini ya Mtandao wa Jinsia nchini TGNP, Saumu Kibasa (kushoto), akitoa maelekezo kwa mwananchi, kuhusu masuala mbalimbali wanayoyafanya, wakati wa kilele cha maadhimisho ya miaka 25 ya Beijing katika Wilaya ya Mbeya, jana. **PICHA GRACE MWAKALINGA**.

## Malezi bora chanzo cha maadili mema

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MALEZI bora ya watoto katika ngazi ya familia yametajwa kuwa ndiyo chanzo cha kuwapo kwa amani, upendo, kuvumiliana na ukarimu katika jamii nchini.

Ofisa kutoka Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Mkoa wa Mbeya, Majid Mohamed, aliyasema hayo jana, jijini hapo alipokuwa anazungumza kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Alisema familia ni kitovu cha ujenzi wa maadili katika jamii kwa kuwa ndiko mwenendo wa tabia za kiongozi huanzia kujengwa kwa kufundishwa na wazazi pamoja na walezi kuhusu maadili mema.

Mohamed alisema kiongozi bora ambaye ni mwadilifu anakuwa na msingi mzuri wa malezi kutoka katika familia yake ambako hufundishwa kuwa mwadilifu, mkweli, mwenye upendo, mwaminifu na mwenye kutambua haki na wajibu.

Alisema maadili hutoa mwongozo wanajamii kuzingatia mambo mema katika uhusiano wao na watu wengine kwenye jamii na kwamba mtu mwenye maadili hupenda mshikamano na amani.

"Kwa asili maadili yanashawishi mtu kufikiria wengine kwa maana ya kuwatendea yale ambayo hata yeye mwenyewe angependa atendewe, sasa ni jukumu la kila familia na jamii kujenga maadili ya mtoto kwa faida ya taifa zima," alisema Mohamed.

Alisema serikali inahitaji watu wengi wenye maadili mema kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo pamoja na kuongoza watu wengine hivyo ni wajibu wa kila mzazi kumlea mtoto wake katika maadili mema.

Kwa upande wake, Lumuli Kibona, alisema kwa sasa kuna tatizo la mmomonyoko wa maadili kwenye jamii kutokana na wazazi wengi kutowafundisha watoto wao mila na desturi za kitanzania ambazo zilitumika kulijenga taifa.

Alisema kwa sasa hata kwenye vyombo vya usafiri wa umma watoto huwa hawana tabia ya kuwaapisha wakubwa kwenye viti hali ambayo inaashiria kuporomoka kwa maadili kwenye jamii.

# CRDB yawakumbuka wanafunzi wa kike taulo za hedhi salama

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

BENKI ya CRDB imeanzisha kampeni maalumu ya kuwasaidia wasichana vifaa vya kujisitiri wakati wa hedhi zikiwamo taulo za kike, ili kuondoa kero ya kutohudhuria masomo wakati wa kipindi hicho.

Hayo yalisemwa juzi wilayani hapa na Meneja wa Benki hiyo Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Feruzi Kolongo, alipokuwa anakabidhi msaada wa taulo za kike zenye thamani ya Sh. milioni tano katika Shule ya Sekondari Madibira.

Alisema utafiti uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) unaonyesha kuwa asilimia 42 ya wasichana ambao huwa hawahudhurii masomo wakati wa hedhi kwa sababu ya kukosa taulo hizo.

Kalongo alisema kutokana na tatizo hilo ndiyo maana benki hiyo iliamua kuanzisha kampeni hiyo ambayo inatekelezwa nchi nzima kwa lengo la kuwasaidia wasichana kupata elimu wakati wote kama ilivyo kwa wavulana.

"Kampeni hii inaitwa 'Hedhi Salama kwa Maendeleo ya Elimu' na inatekelezwa kama sehemu ya kurejesha kwenye jamii sehemu ya faida tunayopata kwenye biashara," alisema Kolongo.

Alisema mbali na kampeni hiyo, benki imekuwa ikisaidia kuboresha miundombinu ya vyoo kwenye baadhi ya shule za sekondari, ili kuwasaidia wasichana kujisitiri kwa maelezo kuwa utafiti wa NIMR pia unaonyesha asilimia 20 ya wasichana wasiohudhuria masomo wakati wa hedhi ni kutokana na miundombinu mibovu ya vyoo.

Akizungumza wakati wa kupokea msaada huo, Mkuu wa Shule ya Sekondari Madibira, Lazaro Malambughi, aliishukuru benki hiyo kwa msaada huo kwa maelezo kuwa utasaidia kupunguza utoro kwa watoto wa kike shuleni hapo.

Malambughi alisema uongozi wa shule hiyo umekuwa ukitumia fedha nyingi kuagiza taulo hizo kutoka maeneo ya mbali kutokana na vifaa hivyo kutopatikana kwenye mazingira hayo.

Alisema shule hiyo ina ya wanafunzi 624 ambao huwa wanahitaji kupatiwa taulo hizo na kwamba baadhi huwa wanatumia vitambaa ambavyo huwa vinatakiwa kufuliwa, lakini tatizo la uhaba wa maji huwa linawafanya wengi kuogopa kuhudhuria shuleni.

"Wanaotumia vitambaa huwa wanatakiwa kuvifua mara kwa mara lakini kutokana na uhaba wa maji wengi huwa wanaamua kutohudhuria shule kabisa, lakini hizi taulo ambazo tumesaidiwa huwa zinachomwa baada ya kutumika na hivyo tatizo la maji halitakuwa shida tena," alisema Malambughi.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdalla, akitembelea kitengo cha maombi ya leseni kwa wafanyabiashara cha Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), jana. **PICHA: OMPR – ZNZ.**

# Makamu wa Pili aanza na wadaiwa sugu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdalla, ameuagiza uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), kuwasilisha ofisini kwake ripoti ya majina ya wadaiwa sugu wote wa madeni ya serikali ndani ya siku saba, ili hatua za kisheria zichukuliwe mara moja dhidi ya wahusika.

Alisema wapo baadhi ya wafanyabiashara na wawekezaji wenye tabia ya kutumia migongo ya wakubwa kukwepa kulipa kodi kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa jambo linalodumaza ukusanyaji wa mapato yanayohitajika kuendesha serikali.

Abdalla alitoa agizo hilo alipofanya ziara juzi Makao Makuu ya Bodi ya Mapato Zanzibar, Mazizini nje kidogo ya Mji wa Zanzibar kuangalia utendaji kazi wa taasisi hiyo ya fedha.

Alisema Bodi ya Mapato ndio tegemeo kubwa la ukusanyaji mapato ya serikali katika kuimarisha uchumi wake na kwamba ipo kazi kubwa ya kuendelea kukusanya kodi hasa kwa wajanja wanaodaiwa kodi na hawana dalili wala mwelekeo wa kulipa au kupunguza madeni yao.

Alitahadharisha kwamba serikali kuu haitasita kuwafutia vibali wawekezaji au wafanyabiashara wote watakaoonyesha dalili ya usugu wa kulipa kodi zao kwa mujibu wa biashara wanazoendesha.

Naye Meneja wa Madeni wa Bodi ya Mapato, Asya Abdisalami, alisema wapo wadaiwa sugu zaidi ya sita wa hoteli na wafanyabiashara wa miradi mikubwa wenye madeni makubwa ya zaidi ya Sh. bilioni 17 yaliyochukua muda mrefu.

Asya alisema, madeni hayo yamejumuisha pia fedha za baadhi ya wafanyakazi wa hoteli kupitia michango yao ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF), pamoja na leseni za biashara.

Kwa upande wake Kamishna wa Bodi ya Mapato, Joseph Abdalla Meza, alisema uongozi wa Bodi ya Mapato umekuwa ukichukua hatua mbalimbali za kuhakikisha madeni hayo yanaendelea kulipwa na pale mhusika anapokaidi maamuzi hayo hufikia hatua ya kufutiwa leseni yake ya biashara.

Meza alisema wapo baadhi ya wadaiwa ambao tayari wamefikishwa kwenye vyombo vya sheria kuhusiana na kukiuka mikataba yao na wengine hujiepusha na adhabu kwa kulipa kadri ya masharti wanayowekewa.

Kamishna huyo alisema uongozi wa taasisi hiyo umechukua hatua ya kukabiliana na mbinu za baadhi ya washirika wao kwa kufunga vifaa vinavyosaidia kuwabaini baadhi ya wawekezaji na wafanyabiashara wanaofuta taarifa kwenye mitandao yao.

Alisema mfumo wa teknolojia unaotumiwa na ZRB hivi sasa unawezesha kutambua taarifa zilizofichwa au kufutwa na wateja na hatimaye uongozi huchukua hatua ya kumwajibisha mhusika kwa mujibu wa kosa alilofanya.

# Jela miaka 3 kwa kumbaka ndugu yake

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA ya Mkoa wa Wete, Pemba, imemhukumu Mansour Salim Mussa (50), jela miaka mitatu na kulipa fidia ya Sh. 200,000 kwa kosa la kumwingilia ndugu yake.

Hakimu wa mahakama hiyo, Abdalla Yahya Shamhun, alisema mahakama imemwona mshtakiwa ana kosa na inamtia hatiani.

Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba, Ali Amour Makame na Juma Mussa, walidai mahakamani hapo kuwa, sio mara ya kwanza kwa mtuhumiwa huyo kutiwa hatiani na mwaka jana alitiwa hatiani kwa kosa la kubaka katika kesi namba 63 ya mwaka 2019.

"Tunaomba mwathiriwa alipwe fidia chini ya kifungu cha 314 cha sheria nambari 7 ya mwaka 2018, Sheria ya Zanzibar," walidai mawakili hao.

Mawakili hao waliiomba mahakama adhabu itolewe kama ilivyo kwenye kifungu alichoshtakiwa cha 143 (1) (2) cha sheria nambari 6 ya mwaka 2018, sheria ya Zanzibar.

Kabla ya kusomwa hukumu hiyo, mtuhumiwa aliulizwa iwapo ana jambo lolote la kuiomba mahakama na alijibu kuwa hana cha kuiomba mahakama.

"Mtuhumiwa utatumikia chuo cha mafunzo kwa muda wa miaka mitatu na utalipa fidia ya Sh. 200,000 na haki ya rufani ipo wazi kwa upande ambao, haujaridhika na maamuzi ya mahakama," alisema hakimu huyo.

Shamhuna alisema, ametoa adhabu hiyo nyepesi kwa vile mshtakiwa anatumikia kifungo cha miaka saba katika kesi ya jinai namba 63 ya mwaka 2019.

Katika kesi hiyo, ilidaiwa mahakamani hapo kuwa, Mansour anakabiliwa na kosa za kumwingilia ndugu yake, kosa ambalo ni kinyume na kifungu cha 143 (1) (4) cha sheria nambari 6 ya mwaka 2018, sheria ya Zanzibar.

# Serikali yaeleza kuwathamini wadau sekta ya elimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imesema inathamini michango mbalimbali inayotolewa na wadau wake katika kuhakikisha inaleta maendeleo endelevu katika sekta hiyo.

Naibu Katibu Mkuu Taaluma wa wizara hiyo, Madina Mjaka Mwinyi, alisema hayo wakati alipofungua mafunzo ya upatikanaji wa takwimu sahihi za majisafi na salama, usafi wa mwili na mazingira katika shule, mafunzo ambayo yamefanyika jana mjini Unguja.

Alisema Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto Duniani (UNICEF), limeandaa mafunzo hayo kwa lengo la kutoa taaluma za namna ya upatikanaji wa taarifa hizo kwa usahihi katika shule za Zanzibar, ngazi za maandalizi, msingi na sekondari kwa kuzingatia mfumo wa taarifa wa Wizara ya Elimu na kuzichambua, kuzitafsiri na kuzitumia kwa mipango ya elimu Zanzibar.

Vile vile, alisema Wizara ya Elimu inathamini mchango huo wa UNICEF kwa kuamua kutoa mafunzo hayo kwa watendaji kutoka taasisi mbalimbali ambayo ana imani kuwa yatawajengea uwezo katika utekelezaji wa majukumu ya kazi zao.

Alisema wizara itahakikisha kuwa mafunzo hayo yanaleta matokeo chanya na yenye ufanisi katika mazingira ya shule kwa kuhakikisha vianzio vya majisafi na salama vinakuwapo katika shule zote na kuwekwa katika hifadhi salama.

Pia alisema wanafunzi watahakikisha kuwa wanakuwapo katika usafi wa mwili na afya njema kupata mabadiliko ya kudumu kuwa na tabia ya kutunza mazingira ya shule, vyoo na vyanzo vya maji.

Alisema kuwapo kwa mafanikio katika sehemu husika kutasababisha kuwapo kwa mazingira mazuri ya watoto ya kujifunza na hivyo kusaidia kuimarika kwa ufaulu wao pamoja na afya zao.

Aliwataka washiriki kutambua kuwa ni muhimu katika kutaarifu taasisi zao na sio kwa UNICEF na kuwataka kushiriki kikamilifu ili wawe mabalozi wazuri wa wenzao katika kuitoa taaluma hiyo.

Alisema kazi ya kuimarisha mifumo ya majisafi na salama, usafi wa mwili na kutunza miudombinu na mazingira ya shule ni kuendeleza malengo ya dunia na kuimarisha maendeleo endelevu na kwamba ni lazima kupewa umuhimu wa kipekee kitaifa ili nchi iweze kutimiza maendeleo yake kwa ufanisi. Madina alitoa shukrani za dhati kwa UNICEF kwa ushiriki wao mkubwa na wa vitendo wa kuisaidia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha kuwa watoto wote wanasoma katika mazingira safi na salama ili kufikia malengo endelevu kwa wote.

Akisoma taarifa ya UNICEF kuhusu mafunzo hayo, Ofisa Maji, Usafi wa Mwili na Mazingira kutokana shirika hilo Zanzibar, Marko Msambazi, alisema mafunzo hayo yanafanyika kwa lengo la kuunda timu ya wataalamu wa kitaifa watakaoendeleza utaratibu wa ukusanyaji wa takwimu ambao ulianza na uimarishaji wa huduma za maji na mazingira katika shule ambao uliingizwa serikalini.

Alisema mafunzo hayo yatasaidia kujua upatikanaji wa takwimu hizo na kumeonekana kuongezeka kwa idadi ya shule pamoja na wanafuzi katika nchi.

Wawezeshaji wa mafunzo hayo walisema, kuna baadhi ya shule ni hatarishi kutokana na miundombinu yake ya huduma za maji na vyoo hasa kwa watu wenye mahitaji maalum na kusababisha kupata matatizo katika kujifunza pamoja na ya kiafya.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:
- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam - 0768 928 516.**
**Arusha - 0677 226 960.**

## NAFASI ZA KAZI

**TANGAZO LA KAZI ,** ANATAFUTWA KIJANA AU DADA ANAYEJUA KUPAMBA KEKI. MALIPO NI MAELEWANO ALIYE SERIOUS ATUME UJUMBE KWENYE **0754 480657 ATAPIGIWA SIMU**

*NIPASHE NI JIBU LAKO*
NJOO UTANGAZE NASI
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**RAPHAEL JUMA SALUMU** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1929-0061** kilichotolewa na shule ya secondary BUKAMBA mwaka 2015, yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Polisi taarifa **DAR/URA/RB/806746/2020**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**HILDA FIDELIS JOB** amepotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajiri **T 482 AYQ** aina yake **NISSAN PATROL.** Yenye chasis namba **JN1TESY61U0006582.** Kwa yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote Cha polisi. Rb namba **MOR/MOR/RB/806645/2020.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No.......Of 2020**

**In the matter of the estate of the late CHONGO ANTHONY MKOKA of Ipagala within Dodoma city**
**And**
**In the matter of Application for letters of Administration by PATRICK ANTHONY MKOKA AND MENHARD ANTHONY MKOKA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 22 day of 10, 2020
Dated at Dodoma this 18 day of 11, 2020

..........................
RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA DISTRIC

1116005402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5**
**KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;348/2020**

**Ombi la GETRUDA JOSEPH,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu EDITHA LAURENT JAKA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/11/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 17/11/2020.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

116005602

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

FEKON COMPANY LIMITED ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 130 CCC.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.

**TAARIFA YA POLISI:**
**MBE/MBE/RB/772580/2020.**

## TAARIFA YA KUFUNGA BEFAO & CO (BFC) LTD

Tunapenda kuutarifu Umma kuwa katika kikao cha Bodi ya Wakurugenzi kilichofanyika tarehe 15/04/2020 kiliazimia kufunga Kampuni ya **Befao & Co (BFC) Ltd** yenye Usajili. No. 135061 kuanzia tarehe **20/04/ 2020.** Kwa maelezo/madai wasiliana na Tel. **0715-388297/0754-388297** au **befao2017@gmail.com**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BENSON ELIAMINI ANDREW** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA SPACIO** yenye namba za usajili **T 980 AFK** chasisi namba **NZE121325147** engine namba **INZB129688** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/KIJ/RB/802566/2020**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;306/2020**

**Ombi la JUMANNE SALUM ULIZA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SAID ATHUMANI NIZOTA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 14/12/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 13/11/2020.

Tarehe 13/11/2020
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;349/2020**

**Ombi la HARRSON SOLOMON MOLLEL,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SOLOMON MOLLEL.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 17/12/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 17/11/2020.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**(JUDICIARY)**

**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MOROGORO**

**SHAURI LA MIRATHI NA. 29/2020**

**RAJABU YASSIN MOHAMED..........................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**YASSIN MOHAMED KIBODYA.....................MAREHEMU**

Mahakama hii inakufahamisha kwamba Mwombaji amefungua maombi yakuwa msimamizi wa mirathi, nakala ya madai hayo yanapatikana katika Mahakama hii.

Shauri limepangwa kutajwa mnamo tarehe 08/12/2020 saa 2:00 asubuhi na kwa yeyote anayehusika na mirathi hiyo anaombwa kufika katika mahakama ya hakimu mkazi Morogoro.
Zingatia kwamba kutokufika kwako tarehe hiyo,Shauri litaanza kusikilizwa bila ya wewe kutaarifiwa tena, na maamuzi kutolewa.

Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 17 mwezi 11 mwaka 2020.

116004502

## TAARIFA YA KUFUNGWA KWA KAMPUNI

**LADRA COMPANY LIMITED** tunapenda kuutarifu Umma kuwa katika kikao cha Bodi ya Wakurugenzi kilichofanyika taarehe **05/11/2020** kiliazimia kufunga kampuni ya **LADRA COMPANY LIMITED** yenye usajili Na **141032** kuanzia tarehe **07/11/2020** maelezo/madai wasiliana namba **0684400542/0715261591** au barua pepe **ladracompanyltd@gmail.com**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF GEITA AT GEITA**

**PROBATE AN ADMINISTRATION CAUSE NO 3 OF 2020**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE THOMAS SHELLO NZOZA**
**AND**
**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR GRANT OF LETTERS OF ADMINISTRATION BY THERESIA THOMAS SHELLO**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner. Objections to the grant should be filed on or before the 18th day of December, 2020. The will of the said deceased is deposited and open for inspection at the Court. Dated at Geita this 12th day of November, 2020.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE
GEITA.

216004402

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

NJOO
UTANGAZE BIDHAA YAKO

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Kenya yaukamata mtandao kuiba watoto

**Nairobi, KENYA**

POLISI nchini Kenya imesema kuwa imebaini mtandao unaohusika na wizi wa watoto katika Jiji la Nairobi nchini Kenya.

Sakata hii imebainika baada ya kipindi cha uchunguzi cha BBC Africa Eye kupeperushwa hewani ambacho kilionyesha uhalifu unaotendeka katika maeneo mbalimbali na hospitali za umma.

Maofisa watatu wa matibabu wa hospitali za umma wamekamatwa na polisi na imedokeza kuwa bado kuna wengi ambao wanatafutwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Inspekta Generali wa Polisi, Hillary Mutyambai, ilisema uchunguzi na taarifa kutoka kwa washirika umeonyesha maofisa waandamizi wa matibabu wanahusika kwa kiasi kikubwa na wizi wa watoto.

Mamlaka imeahidi kuboresha ulinzi wa watoto.

Katika mkutano na waandishi wa habari serikali iliweka wazi kuwa wahusika wa biashara hiyo haramu, wauzaji na wanaonunua watafikishwa katika mikono ya kisheria.

Waziri wa kazi na masuala ya jamii, Simon Chelugui, alisema uchunguzi wa uhalifu huo unaendelea.

Alisema ni muhimu kuboresha huduma ya usalama kwa watoto, serikali haiwezi kuvumilia vitendo hivi vya kinyama.

BBC Africa Eye iliingia kwenye safu ya mitandao haramu, ikishuhudia watoto wakiibiwa kutoka kwa mama wasio na makazi na kuuzwa mitaani kwa kima cha dola za Kimarekani 450.

Mtoto wa kiume anaweza kuuzwa kwa dola 3,000 za kimarekani. Lakini biashara hii ya kusikitisha haishii hapo.

Pia umebainika ushahidi wa watoto waliozaliwa wakiuzwa katika kliniki haramu, na watoto waliotelekezwa wakiuzwa na wafanyakazi wa afya katika Hospitali ya Mama Lucy Kibaki jijini Nairobi. Usimamizi wa hospitali haukujibu madai hayo.

**BBC**



Watoto wakiwa wamekaa chini ya vifusi kwenye nyumba iliyoharibiwa na kimbunga kiitwacho Iota, Puerto Cabezas, nchini Nicaragua. **REUTERS**

# Biden kukutana washauri wa usalama

**Washington, MAREKANI**

RAIS mteule wa Marekani, Joe Biden, amekutana na washauri wake wa usalama wa taifa katika mkutano ambao haukuhudhuriwa na wataalamu wa upelelezi wa serikali, wakati Rais Donald Trump anaendelea kuzuia mchakato wa kipindi cha mpito.

Biden na makamu wake Kamala Harris wamejadili kuhusu masuala mbalimbali ulimwenguni katika mkutano huo na maofisa wa ujasusi na wataalamu wa ulinzi.

Kati ya waliohudhuria mkutano huo ni aliyekuwa Naibu wa Waziri wa Mambo ya Nje, Tony Blinken, waliokuwa mabalozi wa Marekani Nicholas Burns na Samantha Power; generali mstaafu Stanley McChrystal, miongoni mwa wengine.

Katika siku za karibuni, wabunge kadhaa wa Chama cha Republican wamesema kwamba maofisa ujasusi wa serikali, wanastahili kutoa taarifa hizo kwa Biden, kuelekea Januari 20, siku ambayo anatarajiwa kuapishwa.

Rais Donald Trump ameendelea kudai kwamba alishinda uchaguzi mkuu wa Nov 3 na kwamba kulifanyika udanganyifu katika uchaguzi huo, bila kutoa ushahidi wowote.

Kesi kadhaa ambazo amewasilisha mahakamani kupinga matokeo hayo ya uchaguzi, zimetupiliwa mbali kwa kukosa ushahidi.

**VOA**

# Marekani kuondoa wanajeshi

**Afghanistan, IRAQ JANUARI**

KUANZIA Januari 15, 2021, idadi ya wanajeshi wetu nchini Afghanistan itakuwa 2,500.

Naibu Katibu wa Ulinzi wa Marekani, Christopher Miller ametangaza kuwa nchi yake itapunguza idadi ya wanajeshi nchini Afghanistan na Iraq hadi 2,500 kufikia Januari 15, 2021.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Wizara ya Ulinzi (Pentagon), Miller, alisema;

"Kuanzia Januari 15, 2021, idadi ya wanajeshi wetu nchini Afghanistan itakuwa 2,500. Idadi ya wanajeshi wetu nchini Iraq pia watakuwa 2,500 kufikia Januari 15."

Christopher Miller amesema kuwa uamuzi wa Rais wa Marekani Donald Trump unaambatana na vipaumbele vya usalama wa kitaifa na unategemea miezi ya kushauriana na timu ya usalama wa kitaifa.

Miller amesema kuwa anashauriana na viongozi wa nchi nyingi washirika, haswa Katibu Mkuu Jens Stoltenberg na Rais wa Afghanistan, Ashraf Ghani.

Akisisitiza kwamba watamaliza vita ambavyo vilianza na uvamizi wa Afghanistan na Iraq baada ya mashambulizi ya Septemba 11, 2001, Christopher Miller amesema, "Tutaokoa watoto wetu kutoka kwenye mzigo mzito wa vita hivi vya milele."

Mshauri wa Usalama wa Kitaifa wa Marekani Robert O'Brien alisema katika taarifa yake Ikulu.

"Wanajeshi waliosalia Iraq na Afghanistan watalinda balozi zetu na taasisi zingine za serikali ya Marekani katika maeneo haya. Wanajeshi hawa watatetea wanadiplomasia wetu na kumfukuza adui. Rais Trump anatumai kuwa wanajeshi wote katika nchi hizi watakuwa nyumbani salama ifikapo Mei."

**TRT**

# WHO: Ebola imekwisha DRC

**Kinshasa, DRC**

JAMHURI ya Kidemokrasia ya Congo imesema kuwa sasa nchi hiyo imeondokana na ugonjwa wa ebola baada ya siku zaidi ya 40 bila kuripotiwa kwa ugonjwa huo.

Mlipuko wa hivi karibuni kaskazini magharibi mwa nchi hiyo, ulikuwa wa tatu katika kipindi cha miaka miwili.

Lakini chanjo na tiba zilizobuniwa wakati wa majanga yaliyotangulia sasa hivi zinatoa matumaini kwa wagonjwa.

Tangu mwaka 2018, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo imekabiliwa na milipuko ya ugonjwa wa ebola kufuatana.

Mwanzoni mwa Juni wagonjwa kadhaa walipatikana na ugonjwa huo katika eneo la Mbandaka.

Watu 130 waliambukizwa ugonjwa huo, huku 55 kati yao walifariki dunia.

Visa vya ugonjwa huo eneo la Mbandaka vilibainika wakati mlipuko wa ebola mashariki mwa nchi hiyo unakaribia kufikia ukomo wake.

Zaidi ya watu 2,000 walikufa kutokana na ugonjwa huo katika mikoa ya Kivu Kaskazini na Ituri kwa zaidi ya miaka miwili. Huo ulikuwa mlipuko wa pili mkubwa zaidi duniani.

Shirika la Afya Duniani limeidhinisha chanjo iliyotolewa na kampuni ya dawa ya Merk ambayo imetolewa kwa watu 400,000 kote nchini humo.

Mwezi uliopita, Shirika la Dawa nchini Marekani limeidhinisha dawa ya Inmazeb kama tiba ya ebola, baada ya kufanyiwa majaribio huko Congo.

**BBC**



# MESSI
## AKUNWA NA USHINDI ARGENTINA

**LIMA, Peru**

LIONEL Messi amesifia kiwango cha Argentina dhidi ya Peru na anaamini wanaendelea kuwa imara.

Nicolas Gonzalez na Lautaro Martinez walifunga kipindi cha kwanza mjini Lima Jumanne, na kukinyanyua kikosi hicho cha Lionel Scaloni katika ushindi wa tatu katika mechi nne za kufuzu Kombe la Dunia mwaka 2022.

Argentina waliendeleza wimbi la kutofungwa katika mechi 11, huku wakiwa wameshinda mechi zao tatu za ugenini za kufuzu kitu ambacho hawakuwahi kukifanya tangu mwaka 2000.

Messi alifurahishwa na kiwango cha Argentina, ambacho kilikuja siku tano baada ya kutoka sare na Paraguay.

"Nina furaha na ushindi, tulihitaji ushindi huu baada ya mchezo tuliocheza siku iliyopita," alisema nyota huyo wa Argentina kupitia ukurasa wake wa Twitter.

"Tangu mwanzo tulikuwa na mchezo mzuri, mabao yalikuja na tulitengeneza nafasi nyingi za kufunga."

Messi aliongeza: "Kipindi cha pili katika mchezo uliopita pia kilikuwa kizuri na tumeendeleza morali ileile.

"Nafikiri hii ndio njia tunayotakiwa kwenda. Kidogo kidogo tunaendelea kuwa imara kama kundi."

Messi alicheza mechi yake ya 142 kwa Argentina dhidi ya Peru, akiifikia rekodi ya gwiji wa Brazil, Cafu wakishika nafasi ya tano kwa kucheza mechi nyingi zaidi kwa timu ya taifa kwa Bara la Amerika Kusini.



## ARTHUR AONA MWEZI BRAZIL

**MONTEVIDEO, Uruguay**

ARTHUR 'ameona mwezi' Brazil, baada ya kufunga kwa mara ya kwanza huku akielezea goli lake la kwanza la kimataifa baada ya kuisaidia nchi yake kuendelea na mwanzo mzuri wa kufuzu michuano ya Kombe la Dunia wakati wakishinda dhidi ya Uruguay.

Kiungo huyo wa Juventus alifunga bao la ufunguzi dakika ya 34 hapa Montevideo, ambapo Richarlison akaongeza la pili na Edinson Cavani akafunga la kufutia machozi kwa wenyeji, Jumanne.

Kikosi hicho cha Tite kilipata ushindi wake wa nne katika mechi nne za mwanzo za kufuzu Kombe la Dunia mwaka 2022, huku wakiendeleza rekodi ya kutofungwa mechi na Uruguay katika 11.

Baada ya kufunga bao lake la kwanza akiwa na jezi za Brazil, Arthur alifurahishwa kwa mchango wake huo kwa timu ya taifa.

"Nafikiri lilikuwa goli muhimu kufunga. Kwa upande wangu, jambo la muhimu ni kupata nafasi ya kucheza na kuweza kuisaidia timu," alisema.

"Goli lilikuwa zuri na kiwango kilikuwa cha kuvutia na kwa hakika kabisa tulihitaji ushindi."

Brazil inaongoza kwa pointi mbili kileleni dhidi ya wapinzani wao wa bara hilo, Argentina kwenye mbio za kufuzu Kombe la Dunia.

## DESCHAMPS: PAUL POGBA ATAREJESHA MAKALI UTD



**PARIS, Ufaransa**

KOCHA wa timu ya Taifa ya Ufaransa, Didier Deschamps ana matumaini kiwango cha Paul Pogba wakati wa mapumziko ya mechi za kimataifa kinaweza kumsaidia pale Manchester United.

Akiwa na wakati mgumu kule kwa miamba wa Ligi Kuu ya England, Pogba alicheza kwa dakika zote 90 wakati Ufaransa ikiibuka na ushindi wa mabao 4-2 dhidi ya Sweden kwenye Ligi ya Mataifa ya UEFA, Jumanne.

Deschamps alimsifia Pogba na ana matumaini kiungo huyo anaweza kuchukua kiwango hicho cha mechi za kimataifa atakaporudi kule United.

"Sitaki kumshutumu yeyote... lakini namjua yeye, najua namna gani alivyo. Anajisikia fahari, lakini muhimu zaidi ni kwamba ana kipaji," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Wakati anapohitaji kulinda, analinda. Anatoa pasi za mwisho. Paul ni mchezaji wa daraja la juu. Natumaini kiwango chake na sisi kitamsaidia."

Pogba bado hajafunga bao lolote au kutoa pasi ya mwisho katika mechi saba za Ligi Kuu msimu huu.

Ufaransa tayari imefuzu kwenye fainali ya makundi ya Ligi ya Mataifa ya UEFA, na ushindi wao dhidi ya Sweden uliwafanya kupata ushindi wa tano katika ya mechi sita kwenye Kundi lao la A3.

HABARI MICHEZO



# DE BRUYNE
## AMTETEA WALKER KUVURUNDA CITY

**MANCHESTER, England**

KEVIN De Bruyne amemkingia kifua beki wa pembeni wa England na Manchester City, Kyle Walker (pichani), baada ya Roy Keane kumsema vibaya kutokana na kiwango chake alichoonyesha mwishoni mwa juma lililopita wakati wa mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Liverpool.

Katika mchezo huo Walker alisababisha mkwaju wa penalti uliopigwa na Mohamed Salah na kuifanya Liverpool kuongoza kwa muda wa dakika 13, kabla ya Manchester City kusawazisha kupitia kwa Gabriel Jesus dakika ya 31.

De Bruyne ambaye ni mchezaji wa Man City, amesema Walker ni mchezaji wa kipekee na wa tofauti sana kwenye kikosi chao, hivyo halikuwa jambo jema kutupiwa lawama.

"Ni miongoni mwa wachezaji ambao ni wagumu sana kukumbana na majeraha, ni tegemeo na anajua nini maana halisi ya kukaba," alisema.

"Huwezi kumfananisha Kyle na Trent Alexander-Arnold wa Liverpool kwa sababu ni wachezaji wawili tofauti. Trent ni mchezaji anayeweza kushambulia na Kyle huwa anaweza kucheza kwa kushambulia na kuzuia," aliongeza.

Keane ni miongoni mwa wachambuzi wachache waliosema hadharani kuhusiana na Walker kuwa hajifunzi licha ya kucheza soka kwa muda mrefu, lakini De Bruyne alisema Walker hajaliweka suala hilo katika kichwa chake na ni jambo la kawaida upande wake.

"Roy Keane ni mtu wa tofauti sana na kila mtu anafahamu hilo, lakini huo ni mtazamo wake na naamini Walker atakuwa sawa baada ya mapito haya na hajachukulia kauli hiyo kama sehemu ya lawama bali ni sehemu ya changamoto."

Walker alijiunga Manchester City Julai, 2017 kwa dau la euro milioni 52.

## KLABU BINGWA DUNIA YASOGEZWA MBELE

**NYON, Uswisi**

SHIRIKISHO la Soka la Kimataifa (Fifa), limesogeza mbele muda wa mashindano ya Kombe la Klabu Bingwa Dunia hadi Februari mwaka 2021 kutoka Desemba.

Kusogezwa mbele kwa muda wa mashindano hayo ni kutokana na mlipuko wa janga la virusi vya corona.

Wawikilishi wa Bara la Ulaya wanajulikana kuwa ni Bayern Munich baada ya kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya Agosti mbele ya Paris St-Germain, lakini janga la Covid-19 limeathiri baadhi ya mabara na kushindwa kutoa bingwa.

Licha ya kubadilika kwa muda wa kufanyika kwa mashindano hayo, lakini sehemu ni ile ile Qatar kuanzia Februari Mosi hadi 11, mwakani.

Anayeshikilia taji hilo ni Liverpool baada ya kulitwaa Desemba mwaka 2019.

CLUB WORLD CUP QATAR 2019



## PEDRI AISHUKURU REAL MADRID KUTOMSAJILI

**BARCELONA, Hispania**

PEDRI ameishukuru Real Madrid kwa kutomsajili yeye, akisema amekuwa sehemu ambayo alitaka kuwapo pale Barcelona.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17, alijiunga na miamba hao wa LaLiga Januari akitokea Las Palmas, na amefunga mabao mawili katika mechi 10 alizoichezea Barca msimu huu.

Lakini mambo yalikuwa tofauti kwa kinda huyo, ambaye alikataliwa na Madrid baada ya majaribio.

Pedri, ambaye ni nyota wa timu ya Taifa ya Vijana ya Hispania, amesema alishukuru kukataliwa na wapinzani hao wa Barca.

"Nilikwenda kufanya majaribio na Real Madrid, lakini waliniambia sipo kwenye daraja lao," alisema akiiambia Cadena SER.

"Namshukuru yule aliyeniambia sina thamani ya kuichezea timu ile, sasa nipo kwenye timu ambayo mara zote nimekuwa nikipenda."

Barcelona wapo nafasi ya nane kwenye msimamo wa LaLiga, wakipitwa pointi tisa na vinara Real Sociedad, ingawa wana michezo miwili mkononi.

Pedri, ambaye ameanza katika mechi tatu za ligi msimu huu, anafurahia kupata nafasi ya kucheza pamoja na mshindi mara sita wa Ballon d'Or, Lionel Messi.

"Bila shaka nilikuwa na ndoto ya kucheza na Messi, kama ilivyo kwa watoto wengi," alisema.

Barcelona wanarudi dimbani kwenye Ligi Kuu Jumamosi kwa kucheza na Atletico Madrid, Jumamosi.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# UPAMECANO AZIINGIZA VITANI LIVERPOOL, UNITED

## Licha ya kuelezwa kuwapo upinzani mkali wa kumpata, taarifa zimeeleza anaweza kwenda...

**LIVERPOOL, England**

MABINGWA wa Ligi Kuu England, Liverpool wameingia kwenye vita moja na Manchester United ya kumwania beki wa kati kutoka nchini Ufaransa, Dayot Upamecano.

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp, amemtaja beki huyo mwenye umri wa miaka 22, kama chaguo lake la kwanza baada ya kuumia kwa Joe Gomez alipokuwa akiitumikia timu ya Taifa ya England.

Kuumia kwa Gomez kumeongeza matatizo katika safu ya ulinzi ya Liverpool, na kusababisha Klopp kujipanga kuingia sokoni wakati wa dirisha dogo la usajili mapema mwakani.

Gazeti la Athletic liliripoti kuwa Upamecano anaongoza katika orodha ya Klopp, hasa baada ya kuumia kwa Gomez aliyeungana na Virgil Van Dijk katika chumba cha wachezaji majeruhi.

Liverpool iliripotiwa kutaka kumsajili Upamecano msimu ujao, lakini sasa watahitaji kumsajili mapema kuziba pengo lililopo.

Hata hivyo, Liverpool watapata upinzani katika harakati za usajili wa beki huyo wa klabu ya RB Leipzig ya Ujerumani, baada ya benchi la ufundi la Manchester United kuonyesha dhamira ya kumtaka pale kwenye dimba la Old Trafford.

Man United wamejipanga kumsajili Upamecano, ikiwa ni sehemu ya kutaka kuboresha kikosi chao, ili kurejesha heshima kama ilivyokua zamani.

Kwa mujibu wa ripoti, Liverpool inaongoza kwenye mbio za kuwania saini ya mlinzi huyo na kuna uwezekano mkubwa wa kumnasa wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari.

"Upamecano anaweza kwenda Liverpool na dalili zinaonyesha wazi," alinukuliwa mmoja wa watu wa karibu wa wakala wa mchezaji huyo na gazeti la Daily Mail.

Liverpool wanapambana kuhakikisha kwamba wanapata mtu wa kuziba pengo kwenye safu yao ya ulinzi baada ya kukumbwa na majeruhi na kwa vyovyote, lazima waingie sokoni Januari.

## KWA UFUPI

**BALOTELLI KURUDI ENGLAND**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester City na Liverpool, Mario Balotelli, amefanya mazungumzo na timu ya Barnsley. Muitaliano huyo mwenye umri wa miaka 30, yuko huru baada ya mkataba wake na Bresica kusitishwa kutokana na kutohudhuria mazoezi. ***(Sun)***

**XHAKA, ERIKSEN KUPISHANA**

ARSENAL wanaangalia uwezekano wa kufanya mkataba wa kubadilishana wachezaji na Inter Milan, ambao utamwezesha Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 28 kujiunga na Washikabunduki hao na kiungo wa kati, Granit Xhaka mwenye miaka 28, kuhamia katika klabu hiyo ya Italia. ***(Corriere dello Sport, via Talksport)***

**CHELSEA WAMTAKA BELLINGHAM**

CHELSEA wanataka kusaini mkataba na kiungo wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham, mwenye umri wa miaka 17, badala ya kiungo wa kati wa West Ham Declan Rice, 21. ***(Eurosport)***

**GUARDIOLA BADO HAKIJAELEWEKA**

KOCHA Pep Guardiola bado hajaamua kuhusu hatima yake ya baadaye pale Manchester City. Mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Goal)***

**LEICESTER WAMWANIA MENDES**

KLABU ya Leicester City inamfuatilia kwa karibu Nuno Mendes mwenye umri wa miaka 18, ambaye anakipengele kinachomruhusu kununuliwa kwa pauni milioni 40 katika mkataba wake na Sporting Lisbon. ***(Mail)***

**POGBA AITWA JUVENTUS**

KIUNGO wa kati wa zamani wa Juventus, Claudio Marchisio, amemtaka mchezaji wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 27, kurejea katika klabu hiyo ya Italia. ***(Mirror)***

**ARSENAL KUMUUZA SALIBA**

ARSENAL wako katika mazungumzo ya kumtoa kwa mkopo beki Mfaransa William Saliba msimu ujao. ***(Evening Standard)***

**UNITED KUSAJILI JANUARI**

MANCHESTER United wameweka nia ya kutaka kufanya usajili Januari, huku Phil Jones mwenye umri wa miaka 28, Sergio Romero (33) na Marcos Rojo (30), wakiwa na uwezekano mkubwa wa kuondoka katika klabu hiyo. ***(Manchester Evening News)***

**TRAORE AIGOMEA WOLVES**

MAZUNGUMZO ya kuongeza mkataba kati ya Wolves na winga Adama Traore yamekwama kwa sababu raia huyo wa Hispania hafurahii muda anaopewa kucheza mechi. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 24 awali alihusishwa na taarifa za kurudi Barcelona. ***(Goal)***

**WEST HAM SAFI KWA DIAZ**

KLABU ya West Ham wamepewa ofa ya kusaini mkataba na mshambuliaji wa Real Mdrid, Mariano Diaz mwenye umri wa miaka 27.

**CONTE AMTAJA VAN DIJK**

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Antonio Conte, amesema alitaka kuwasajili mlinzi wa Liverpool, Virgil van Dijk na mshambuliaji Romelu Lukaku wa Inter Milan wakati akiinoa klabu hiyo. ***(Telegraph)***



HABARI MICHEZO

# MOROCCO AFUNGUKA KUTUA NAMUNGO FC

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes), Hemedi Suleiman Morocco, amesema bado hajasaini mkataba wa kuitumikia Namungo FC inayoshiriki Ligi Kuu Bara, lakini wanaendelea na mazungumzo.

Morocco anatarajiwa kurithi mikoba ya Thiery Hitimana, ambaye aliachwa jijini Dar es Salaam katika msafara wa kuelekea Zanzibar kuweka kambi kutokana na kikosi hicho kutokuwa na matokeo mazuri kwenye mechi 10 za Ligi Kuu Bara msimu huu.

Namungo imeweka kambi yake visiwani humo kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Yanga utakaochezwa Jumapili pamoja na mechi ya kwanza ya kimataifa ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Rabita FC ya Sudan Kusini.

Akizungumza na gazeti hili jana, Morocco alisema bado hajaanza kukinoa kikosi hicho, lakini mazungumzo yatakapokamilika, ataanza kazi hiyo mara moja.

Morocco alisema mpira ndio kazi yake na hatasita kujiunga na klabu yoyote iwe Tanzania Bara au visiwani, endapo watafikia makubaliano.

"Tumekuwa na mazungumzo ya zaidi ya wiki mbili, kama yatakamilika na kunitangaza rasmi nitaungana nao, kwa sasa bado sijaingia mkataba nao," alisema kocha huyo.

Katibu Mkuu wa Namungo, Ally Suleiman, alisema taarifa rasmi kuhusiana na hatima ya Hitimana itajulikana leo.

"Taarifa rasmi inatarajiwa kutolewa kesho (leo) na Mwenyekiti wa timu (Hassan Zidadu), ambaye ndiye alitoa amri ya Hitimana kutokwenda na kikosi visiwani humo, kwa sasa timu iko chini ya Kocha Msaidizi, Gogfrey Okoko," alisema katibu huyo.

Aliongeza kuwa, katika kuendelea kujiimarisha, timu yao inatarajia kucheza mechi ya kirafiki na klabu mojawapo ya Ligi Kuu Zanzibar ambayo wanaamini itawajenga.

Hitimana aliliambia gazeti hili amebaki jijini na anatarajia kukutana na mwenyekiti wa timu hiyo kwa lengo la kupokea maelekezo.

"Bado sijakutana na mwenyekiti, hivyo sitaweza kuzungumza lolote, kama ni kuhusu kufutwa kazi hilo ni jambo la kawaida kwa kocha yeyote kukabiliana na hali atakayokutana nayo," alisema Hitimana.

Hitimana ambaye aliipandisha timu hiyo amekuwa na mwanzo mbaya msimu huu wakati msimu wake wa kwanza katika Ligi Kuu Bara aliisaidia klabu hiyo kumaliza nafasi ya tano.

Namungo itaikaribisha Al Rabita FC katika mechi ya kwanza ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika Novemba 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, uliopo Chamazi jijini.



DUH!...

Wachezaji wa Taifa Stars, wakishindwa kuamini kilichotokea baada ya kutangulia kufungwa na Tunisia wakati timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1 katika mechi ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2022, kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi usiku. **MPIGAPICHA**

# Ngorongoro Heroes kamili Arusha

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha Timu ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes), kimewasili salama Arusha na kiko tayari kwa mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-20), yatakayoanza Jumapili hadi Desemba 2, mwaka huu jijini humo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Ngorongoro Heroes, Jamhuri Kihwelo 'Julio', alisema wanatarajia kuendelea na mazoezi leo baada ya kuwapa mapumziko ya siku moja ya kuondoa uchovu wa safari.

Julio alisema wamejiandaa kufanya vema kwenye michuano hiyo na wanaamini watalinda heshima ya Tanzania katika mashindano hayo.

Kocha huyo alisema amesafiri na wachezaji 25 na wamevutiwa na hali ya hewa na uwanja ambao watautumia kwenye michuano hiyo inayotarajiwa kushirikisha nchi tisa.

"Tuliondoka Dar es Salaam jana (juzi) usiku, tumefika salama, niko na kikosi cha wachezaji 25, ila tutamkosa Ally Msengi ambaye amerejea katika klabu yake, lakini wachezaji wengine wanaocheza nje akiwamo Kelvin John wapo," Julio alisema.

Ngorongoro iliyoko Kundi A itafungua pazia la michuano hiyo Jumapili dhidi ya yosso wenzao wa Djibouti na itamaliza hatua ya makundi Novemba 26, mwaka huu kwa kuwavaa Somalia.

Kundi B katika mashindano hayo linaundwa na Burundi, Sudan Kusini na Uganda huku Ethiopia, Kenya na Sudan wakiwa Kundi C.

## Biashara United yaitisha Dodoma

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Biashara United, Francis Baraza, amesema kikosi chake kipo 'fiti' na tayari kuwakabili Dodoma Jiji FC katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Samora mkoani Iringa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Baraza alisema anaufahamu ubora wa wapinzani wao na ameyafanyia kazi makosa yaliyoko katika kikosi chake ikiwamo safu ya ushambuliaji na ulinzi ambayo bado haijakaa vema.

Baraza alisema katika kufanyia kazi safu hizo mbili, ameongeza nguvu kwa kuwapandisha wachezaji wawili kutoka katika kikosi cha vijana ambao ni mshambuliaji, Isdory Jackson na beki wa kulia, Dennis Mkami.

"Baada ya kuridhishwa na viwango vya nyota hao, nina imani watasaidia timu yangu kuelekea mchezo wetu huo dhidi ya Dodoma FC, itakuwa mechi ya ushindani kwa sababu sisi sote tunahitaji kupata matokeo mazuri," alisema Baraza.

Kocha huyo alisema alikuwa na tatizo la mabeki wake kupoteza umakini na kuruhusu mabao dakika za mapema, amefanyia kazi na anaamini makosa hayo hayatajirudia katika mchezo huo.

Mechi nyingine za Ligi Kuu Tanzania Bara zitakazochezwa kesho ni kati ya Ruvu Shooting dhidi ya Mbeya City wakati Mtibwa Sugar watawafuata Ihefu kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga.

## KMC FC kamili kuwavaa Azam

**Na Saada Akida**

BAADA ya nyota wake waliokuwa kwenye majukumu ya kimataifa kurejea, uongozi wa KMC FC umesema kikosi chao kimekamilika na kipo tayari kuwavaa Azam FC katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa KMC, Christina Mwagala, aliliambia gazeti hili wachezaji waliorejea kwenye kikosi chao ni pamoja na nahodha, Juma Kaseja na David Brayson waliokuwa kwenye Timu ya Taifa (Taifa Stars), iliyokuwa inakabiliwa na mechi mbili za kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Kombe la Afrika (Afcon) 2022 dhidi ya Tunisia.

Mwagala alimtaja mwingine aliyerejea kwenye timu yao ni kocha wa magolikipa, Fatuma Omary ambaye alikuwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars) na (U-17), zilizokuwa katika michuano ya COSAFA nchini Afrika Kusini.

Alisema timu hiyo inaendelea kufanya mazoezi na wanaamini wataondoka na matokeo chanya na kurejea kwenye kasi waliyoanza nayo msimu huu.

Aliwataja wachezaji ambao hawataonekana katika mchezo huo kuwa ni Pic Ally ambaye alifiwa na baba yake mzazi pamoja na Rahim Sheihe aliyeko katika Timu ya Taifa ya Vijana (Ngorongoro Heroes), ambayo ipo Arusha kwenye mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa U-20).

Alimtaja nyota, Emmanuel Mvuyekule aliyekuwa majeruhi kuwa ameshareja mazoezini na mwalimu anaweza kumtumia katika mchezo unaofuata endapo ataamua kufanya hivyo.

# Michezo

Alhamisi Novemba 19, 2020

Nipashe




UPAMECANO AZIINGIZA VITANI LIVERPOOL, UNITED HABARI UK 22

TULIA...



Beki wa Peru akimvuta mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi, baada ya kushindwa kumdhibiti kwenye mechi ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia Ukanda wa Amerika Kusini iliyopigwa Uwanja wa Taifa wa Lima usiku wa kuamkia jana. Argentina ilishinda 2-0 kwa mabao ya Nicolas Gonzalez dakika ya 17 na Lautaro Martinez dakika ya 28. **PICHA: MAKTABA**

# YANGA SC WAANZA KUSHIKANA 'UCHAWI'

## Mzimu wa hujuma wamwangukia Kaimu Katibu Mkuu, asimamishwa kazi, Morrison atajwa...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Klabu ya Yanga ikiwa kwenye vita ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao wameukosa kwa misimu mitatu mfululizo, 'moshi mweusi' umeanza kufuka kwenye klabu hiyo baada ya kuanza kushikana 'uchawi' kutokana na kutangaza kumsimamisha kazi Kaimu Katibu Mkuu wao, Simon Patrick.

Kiongozi huyo ambaye ni Mkurugenzi wa Sheria na Wanachama, amesimamishwa kuendelea na majukumu yake baada ya kikao cha Kamati ya Utendaji ya Yanga kilichofanyika juzi jijini Dar es Salaam kumkuta na tuhuma mbalimbali.

Taarifa rasmi iliyotolewa na Yanga jana, ilieleza kikao hicho kilifanyika maalumu kwa ajili ya kusikiliza tuhuma (hazijawekwa wazi), zilizokuwa zinamkabili kiongozi huyo, na hivyo kufikia uamuzi huo ili kutenda haki.

"Kwa dhumuni la kuhakikisha haki inatendeka, Kamati ya Utendaji itateua Kamati Huru kuchunguza suala hili na kutoa uamuzi wenye tija kwa pande zote. Hivyo Kamati ya Utendaji itasubiri Kamati Huru kukamilisha uchunguzi wake na kutoa ripoti ya juu ya tuhuma hizo," ilisema sehemu ya taarifa.

Habari za ndani zinasema Simon amekuwa akitofautiana na baadhi ya viongozi wa klabu hiyo katika mambo mbalimbali na hivyo kuonekana si mwadilifu.

Mmoja wa wajumbe, Athumani Kihamia, alionekana hadharani akimtuhumu Simon kwamba anatumika kuihujumu Yanga, jambo ambalo linaweza kuigharimu klabu yao kwenye vita ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao unashikiliwa na watani zao, Simba.

Baadhi ya tuhuma zinazomweka pabaya Simon ni kukutwa akiwa na kiongozi wa juu wa Simba na hivyo ukaribu huo umewatia mashaka mabosi wake huku pia akituhumiwa kwa kufuta kesi iliyowasilishwa na Yanga Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) dhidi ya aliyekuwa mchezaji wao, Bernard Morrison.

Tuhuma nyingine iliyoibuliwa ni ya kutopokea simu pale anapopigiwa na Mwenyekiti wa Yanga, Dk. Mshindo Msolla, jambo ambalo alilikanusha na kueleza, huwasiliana zaidi na kiongozi huyo wa juu kuliko mtu mwingine yeyote ndani ya klabu hiyo.

Pia imedaiwa kuwa eti Simon anahofia nafasi yake kuchukuliwa na Senzo Mazingisa, ambaye alijiunga na Yanga kama mshauri wa klabu hiyo kuelekea kuendeshwa kwa mfumo mpya, wakati akitokea Simba kama Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu.

# NDAYIRAGIJE: STARS BADO INA NAFASI AFCON 2022

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Etienne Ndayiragije, amesema anatarajia timu hiyo itafanya vizuri katika safari ya kutafuta tiketi ya kufuzu kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) 2022.

Akizungumza na gazeti hili jijini juzi baada ya mechi ya Stars dhidi Tunisia iliyopigwa Uwanja wa Benjamini Mkapa jijini Dar es Salaam, Ngayiragije alisema ameridhishwa na wachezaji walivyopambana na kulazimishwa sare ya kufungana bao 1-1.

Alisema anawapongeza wachezaji wake kupambana na anaamini kwamba kile ndicho kiwango cha timu yake ilipoishia na kwamba kunahitajika muda mrefu wa kuziandaa timu za taifa kama zinavyoandaliwa klabu za Tanzania katika mechi kubwa.

**"Ukiangalia mechi zote mbili wachezaji wetu wamepambana kuanzia ugenini na nyumbani, sasa tunahitaji kupata maandalizi ya kutosha, nina imani ya kufanya vizuri katika mechi mbili zijazo kupata pointi muhimu na kutufanya kusimama katika nafasi nzuri," alisema Ndayiragije.**

Kuhusu mshambuliaji Adam Adam alisema amekiona kitu kwa mchezaji huyo na ana imani ataleta kitu ndani ya kikosi hicho kwa sababu ni mechi yake ya kwanza kucheza akiwa ndani ya Stars.

Kwa matokeo hayo Stars ipo nafasi ya tatu ikiwa na pointi nne baada ya kucheza mechi nne, huku Tunisia ikiwa nafasi ya kwanza kwa pointi 10 ikifuatiwa na Equatorial Guinea yenye alama sita huku Libya ikiburuza mkia na pointi zake tatu kwenye Kundi hilo la J.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002